**Viongozi** matatani tuhuma za wizi wa mamilioni ushirika

UKURASA 3



**Marekani** yamwaga Bil.18.5/- kununua chakula cha wakimbizi

UKURASA 5

Mama Samia alivyoanza siku tano Tanga Ukurasa 12





Ukurasa 13

**Sakaya: Uchaguzi mkuu uliopita umenipa ari ya kujipanga zaidi**



Ukurasa 14

**Kanali Besigye: Swahiba wa Museveni tangu porini, leo wako 'paka na panya'**

**siasa**

JUMATANO MACHI 17, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


# Nipashe

Jumatano Machi 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580522

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


CHIFU NKOSI MHARULE

## Kaburi lake limebeba maajabu, ...ni kote wamiminika kuhiji

• Atoka Afrika Kusini, azikwa na wawili hai



Kaburi la Chifu Nkosi Mharule Bin Zulu Gama. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

ni wengi waliokuwa wanazikwa wakiwa hai na mfalme, ni wale ambao walikuwa wamezoeana na kufanya kazi naye kwa karibu.

Hata hivyo, anaesema kaburi hilo linatumiwa na wananchi wa kijiji hicho kwenda kuhiji kila ...

wa Mharule kutoka Afrika Kusini walifika kushuhudia kusimikwa kwa Chifu Nkosi Imanuel Zulu Gama wa Tano, ambaye ndiyo chifu wa wangoni wa sasa.

Ngonyani anasema yeyote ambaye ...

waliofika kutambika na kupiga magoti juu ya kaburi na kuomboleza kwa sala za jadi.

Hapo Ngonyani ana simulizi zake: "Baada ya maombi, kuku au mbuzi wanachinjwa juu ya kaburi la Chifu Mharule, jambo ...

nye kaburi hilo.

Agnes Ngonyani, kiongozi wa kimila Msaidizi wa Mzee Ngonyani, anasema wamekuwa wakipokea wageni wengi wanaotembelea kaburi la Chifu Mharule kutoka nchi ...

# Sakata la polisi kugawana nyama latua kwa DCI

UKURASA 2



## Ofisa Uhamiaji jela kwa rushwa

UKURASA 3



## Mwanafunzi wa sekondari aiandikia shule kutaka aolewe

UKURASA 2

**MICHEZO** MFARANSA YANGA SASA NI MUDA TU UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Ndugulile ataka unafuu wa tozo usajili mitandao

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ameagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kuangalia upya tozo za usajili wa mitandao ya kijamii.

Sambamba na hiyo, ameitaka TCRA kuboresha kanuni ili zisiwe kikwazo kwa vijana pamoja na kutaka kupunguza gharama za usajili wa kuendesha mitandao ya kijamii ili Watanzania wengi wajiajiri kupitia mitandao hiyo.

Dk. Ndugulile alitoa maelekezo hayo jana jijini hapa baada ya kutembelea taasisi za serikali zilizo chini ya wizara yake.

Akionyesha kutopendezwa na ukali wa matakwa ya kikanuni ya usajili wa mitandao hiyo, Dk. Ndugulile alitoa siku 30 kwa mamlaka hiyo kuzipitia sheria zote na kuhakikisha inaweka wazi muda wa usajili wa mitandao hiyo kuanzia sasa.

Alisema ni vyema mamlaka ikajikita zaidi kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na matumizi yasiyo sahihi ya mitandao hiyo kwa kuwa ni kosa kisheria kutumia mtandao wa kijamii bila kusajiliwa.

Hata hivyo, aliipongeza TCRA Kanda ya Kaskazini kwa kutoa elimu kwa mafundi simu na kusema elimu hiyo itawasaidia kutambulika kisheria na kuzitaka kanda zingine kuiga mfano huo.

"Niwaonye mafundi simu wote wale ambao wanafuta IMEI namba za simu ambazo zimeibiwa na kuweka IMEI namba mpya waache mara moja kwani wizara ina mashine ambazo hata ukifuta simu inatambua," alisema.

Pia alisisitiza kuwa iwapo fundi yeyote atabainika amefanya uhalifu huo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Aidha, aliwataka wananchi kufahamu kuwa ifikapo Juni 30, mwaka huu, laini zote za simu ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole zitafungiwa kwa kuwa serikali ilishatoa muda wa kutosha kwa wananchi kusajili kwa alama za vidole.

Akiwa katika ofisi ya Posta, Waziri huyo aliwataka wafanyakazi kuongeza ubunifu zaidi pamoja na kuongeza ufanisi katika utendaji wao wa kazi. Awali, Meneja wa TCRA Kanda ya Kaskazini, Mhandisi Emelda Salumu, alisema kwa mwaka 2020/21 wana mpango wa kukusanya Sh. bilioni 1.27 na kwamba hadi sasa tayari wamekusanya zaidi ya Sh. millioni 800.

Alisema katika kuhakikisha uhalifu kupitia mitandao ya simu unapungua, wameamua kutoa elimu kwa wananchi pamoja na mafundi simu ambapo mafunzo 332 wamepatiwa katika kanda hiyo.

# Sakata polisi kugawana nyama latua kwa DCI

**Na Romana Mallya**

UCHUNGUZI dhidi ya baadhi ya askari polisi wa Kituo cha Polisi Buguruni jijini Dar es Salaam, kudaiwa kukamata nyama za wafanyabiashara kisha kuzigawana kituoni, umeanza.

Kamanda wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliiambia Nipashe jana kuwa wapelelezi kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) kwa kushirikiana na Mkuu wa Upelelezi Makosa ya Jinai Kanda Maalum ya Dar es Salaam (ZCO), wameshatua kituoni Buguruni kufuatilia suala hilo.

"Nimetoka hapo kituoni (Buguruni), nimemwacha ZCO akisaidiana na Ofisi ya DCI kufuatilia hili.

"Kwa sasa sitalisemea, ninasubiri matokeo ya uchunguzi. Wao (wafanyabiashara) walisema hivyo, lakini hawakuonyesha chochote kinachothibitisha madai yao.

"Tunasema madai ni madai, yanatakiwa kuchunguzwa, linafanyiwa uchunguzi. Tukikamilisha, tutawaambia," alisema.

Juzi, wakati wa kikao kilichowakutanisha maofisa wa serikali, viongozi wa ushirika na wafanyabiashara wa Machinjio ya Vingunguti, zilitolewa shutuma dhidi ya baadhi ya askari wa Kituo cha Polisi Buguruni kuwa wamekuwa wakikamata nyama machinjioni na kugawana kituoni.

Mfanyabiashara Mgendi Matutu, akizungumza wakati wa kikao hicho, alidai alishuhudia askari polisi wakigawana nyama Kituo cha Polisi Buguruni siku moja kabla ya mkutano huo kuitishwa.

"Nilikuwa na nyama za mbuzi wanne waliokuwa kwenye deli nne zikiwa na utumbo wake, zimekamatwa kongoro kozi nne za ng'ombe, ndimi 10, mikia ya ng'ombe mitano.

"Nilikuwa nimetoa mizigo kutoka machinjioni kwa sababu wameshafanya ambushi eneo lililozuiliwa tulilokuwa tunatumia kutengeneza nyama ili kwenda sehemu husika.

"Nikalazimika kwenda bucha jirani. Wakati ninagonga nyama, wakafika wakiongozwa na Msajili wa Bodi ya Nyama wakachukua deli lote," alidai.

Aliendelea kusimulia kuwa baada ya watu hao kuchukua nyama yake, walimwambia aende Buguruni kulipa faini na alipofika kituoni, alikutana na mwenzake ambaye alimweleza kuwa askari wapo jengo la upelelezi wanagawana nyama.

"Nimeokoka, nikasema afadhali niende kuona haki yangu inavyotapanywa. Niliendа na kushuhudia askari na mmoja alikuwapo hapa (kikaoni) anajifichaficha baada ya kuniona kwa sababu nilimkariri na mwingine alikuwa amevaa gwanda na yupo niliyefanikiwa kumjua kwa sababu walimtaja jina, anaitwa Afande Ali, alikuwa na radio call, ninafikiri alikuwa anaongoza kile kikosi," alidai.

Mfanyabiashara huyo alidai kuwa alipofika eneo ambalo askari waliokuwa wakigawana nyama, alihoji kwa nini wanafanya hivyo ndipo alipokamatwa kama mtuhumiwa wa ujambazi.

"Mimi siyo jambazi, ninamtumainia Yesu Kristu, ninatafuta fedha ninaitolea zaka na kutolea sadaka. Mungu nitie nguvu, kilichofanyika nikawekwa chini ya ulinzi. Bahati nzuri alikuwapo mtu mstaarabu kutoka Bodi ya Nyama, akasema nilipe faini kwa sababu suala langu ni dogo," alisema.

Matutu alidai alilipa faini ya Sh. 100,000 kwa njia ya simu, akionyesha nyaraka mbalimbali za malipo hayo, lakini alipoomba mzigo wake, aliambiwa umeteketezwa.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akishika maji baada ya kuweka jiwe la msingi la mradi wa majisafi na salama katika Kijiji cha Pongwe, wilayani Muheza, mkoani Tanga jana. Kulia ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso. **PICHA: IKULU**

# Mwanafunzi wa sekondari aandika barua kutaka ndoa

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Mtwivila mkoani Iringa, amemwandikia barua Mkuu wa Shule hiyo kuomba kuacha shule ili aolewe.

Mkuu wa Shule hiyo, Daines Nyalla, alibainisha mkasa huyo jana mbele ya Diwani wa Mkimbizi, Eliud Mvella, aliyetembelea shuleni huko kujua maendeleo yao.

Alisema mwanafunzi huyo awali alikuwa na tatizo la ukosefu wa sare za shule na yeye (Mkuu wa Shule) alijitolea kumnunulia.

Alisema licha ya kumnunulia nguo, mahudhurio yake hayakuwa ya kuridhisha na walipofuatilia kupitia wanafunzi wenzake na kuitwa shuleni, alionyesha kukataa shule.

"Baada ya siku chache, aliandika barua kueleza kusudio lake la kuacha shule ili kwenda kuolewa," alibainisha.

Mwalimu huyo alisema barua hiyo yenye kichwa cha habari 'yahusu kuacha shule kwenda kuolewa', ilikuwa na maelezo mengi yaliyomsukuma mwanafunzi wake kutaka kuolewa, mengi yakiwa hayana mashiko kimaadili.

Alisema mbali na mwanafunzi huyo, wapo wengine 14 ambao ni watoro na uongozi wa shule unaendelea kuwafuatilia.

Baada ya maelezo hayo, Diwani Mvela aliagiza mwanafunzi huyo na wenzake 14 kusakwa kokote waliko na kurejeshwa shuleni.

HABARI KITAIFA

# Mgomo wa daladala wazidi kushika kasi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADEREVA wa daladala jijini Mbeya, wameendelea na mgomo kushinikiza serikali kuziondoa bajaji kwenye njia zao, huku wakisisitiza hawatarejesha magari barabarani mpaka Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila atakapochukua hatua. Mgomo huo uliendelea jana ikiwa ni siku ya pili na madereva hao walikataa kumsikiliza kiongozi yeyote wa serikali kwa madai kuwa walikuwa wanamtaka Chalamila azungumze nao wakidai wanakerwa na kauli anazozitoa dhidi yao kwenye vyombo vya habari.

Baadhi ya viongozi wa serikali wenye nyadhifa mbalimbali walifika katika Kituo cha Daladala cha Kabwe kwa nia ya kuzungumza na madereva hao namna ya kuumaliza mgomo huo, lakini madereva hao wakawakataa na wakiwataka waondoke. Baadhi ya viongozi waliokataliwa na madereva hao ni Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika.

Baada ya madereva hao kugoma kuwasikiliza viongozi hao, Kamanda Matei aliwachukua viongozi wa chama cha madereva na kwenda kujadiliana nao namna ya kumaliza mgomo huo.

Baadaye viongozi wa Chama cha Madereva walirejea kuwapatia mrejesho wenzao, lakini madereva hao wakaukataa na kutangaza kuendelea na mgomo mpaka Chalamila atakapowasikiliza.

Mwenyekiti wa Nidhamu wa Baraza la Madereva Daladala, Ulimboka Kikosa, alisema walianza kujadiliana na serikali jambo hilo tangu Mei, mwaka jana, lakini mpaka sasa hawajawahi kuonana na mkuu wa mkoa.

Alisema mkuu huyo wa mkoa amekuwa akiwatuma viongozi wa chini yake ili wazungumze nao, lakini yeye anatoa matamko makali kwenye vyombo vya habari ikiwamo kutishia kufuta leseni za biashara za wamiliki wa magari.

"Tunataka mkuu wa mkoa aje kuzungumza na sisi. Hatutaki kiongozi mwingine maana yeye ndiye amekuwa akitamka wazi kwamba hataziondoa bajaji barabarani," alisema Kikosa.

Naye Mjumbe Mshauri wa Chama cha Madereva Daladala, Alfred Mwakibete, alisema wanashindwa kufikia makubaliano kwa sababu madereva bajaji hawazuiwi kuchukua abiria mahali popote, lakini wao wakichukua abiria mahali ambapo hakuna kituo, wanakamatwa na kutozwa faini. Alisema kama serikali inataka daladala na bajaji wafanye kazi kwa pamoja, serikali iache kuwatoza faini wanapochukua abiria kwenye maeneo ambayo hakuna vituo na kusiwe na utaratibu wa kila gari kwenda kwenye njia iliyosajiliwa. Baadhi ya wananchi walisema mgomo huo umeathiri shughuli zao zikiwamo za kiuchumi na kijamii kutokana na kushindwa kufika kwa wakati kwenye maeneo yao ya kazi.

Mmoja wa wananchi hao, Salum Komba, alisema mgomo huo umesababisha gharama za maisha kuongezeka kwa maelezo kuwa kabla ya mgomo, walikuwa wanatumia Sh. 400 ya nauli kutoka Uyole mpaka mjini lakini sasa hivi wanatumia zaidi ya Sh. 2,000.

Alisema kuna baadhi ya wananchi ambao wamekuwa wakienda hospitalini kutibiwa, lakini wanakwama kutokana na gharama kubwa za usafiri na kwamba hata wanafunzi wanahangaika kwenda shuleni.

Hata hivyo juzi Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Chalamila alisema kama madereva hao wataendelea na mgomo huo anaweza akaamuru magari ya serikali yakiwamo ya majeshi kufanya kazi ya kusomba abiria na kufuta vibali magari yaliyogoma.



Wakazi wa Mtaa wa Kichangani, Kata ya Kisarawe Two, Manispaa ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, wakichota maji yasiyo salama kwenye kisima kwa ajili ya matumizi ya nyumbani jana, ambapo wamelalamikia kiwanda cha kutengeneza maturubai, mikeka na vyombo vya plastiki cha Ruida, kwa kutiririsha maji machafu yanayoharibu mazingira ya wakazi wa eneo hilo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ofisa Uhamiaji jela makosa ya rushwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

OFISA Uhamiaji wa Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Silvester Kayani, amehukumiwa kutumikia kifungo cha miezi mitatu gerezani baada ya kupatikana na hatia katika makosa ya rushwa.

Kayani alianza kutumikia adhabu hiyo jana baada ya kushindwa kulipa faini ya Sh. 600,000 alizotozwa na Mahakama ya Wilaya ya Babati kwa kupatikana na hatia ya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 100,000.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya hiyo, Victor Kimario, alisema mshtakiwa huyo ametiwa hatiani baada ya mahakama kujiridhisha pasi na shaka alivunja sheria makusudi kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

"Mahakama hii imekukuta na hatia na inakuhukumu kutumikia kifungo cha miezi mitatu gerezani au kulipa faini ya Sh. 600,000," alisema Hakimu Kimario.

Kesi hiyo namba 81 ya mwaka 2020, ilikuwa ikiendeshwa na Mawakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Martin Makani na Evelyine Onditi.

Awali, katika hati ya mashtaka, ilidaiwa mahakamani huko kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Machi mwaka jana baada ya kushawishi rushwa hiyo kutoka kwa mwananchi mmoja, mkazi wa Babati na mzaliwa wa Singida.

Ilidaiwa kuwa ofisa huyo wa uhamiaji alitaka kupewa rushwa hiyo ili asichukulie hatua kutokana na tuhuma za uhamiaji haramu alizokuwa amezipokea dhidi ya raia huyo.

Baada ya Kayani kuomba rushwa, TAKUKURU iliweka mtego wa rushwa ambao ulisaidia kukamatwa kwa ofisa huyo katika Hoteli ya Royal Beach iliyoko karibu na Ziwa Babati.

# Matatani madai wizi mamilioni ya ushirika

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU watano akiwamo Katibu wa Chama cha Msingi Umoja na Wafanyabiashara, Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, wanashikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa tuhuma za wizi, kughushi na kujipatia Sh. 58,335,260 kinyume cha sheria.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Lindi, Abtery Mganga, alisema hayo alipokuwa anatoa taarifa ya utekelezaji kwa vyombo vya habari.

Aliwataja watuhumiwa hao ni Rahimu Hamisi Tewele (Katibu wa Chama cha Msingi Umoja), Said Ally Tindwa (mfanyabiashara, mkazi wa kijiji cha Mbonde); Abdulatifu Hamisi Tewele (mfugaji, Hawa Salum Pange, wakazi wa Kijiji cha Makonjiganga) na Kuruthum Hassani Mfaume (wakala wa fedha wilayani Liwale).

Mganga amedai watuhumiwa hao, walijipatia fedha hizo msimu wa mauzo ya korosho mwaka 2019/2020, kupitia ghala la Chama cha Msingi Umoja (AMCOS), kwa kuongeza idadi ya kilo za korosho na kujipatia Sh. 58,335,260, hivyo kushindwa kuwalipa fedha wakulima halali.

Kwa mujibu wa Mganga, Tewele akiwa katibu wa chama hicho, alitumia madaraka yake vibaya na kinyume cha sheria kwa kughushi nyaraka na kuingiza majina hewa ya wakulima, huku akijua watu hao hawakuwahi kuuza korosho kwenye chama katika msimu 2019/2020.

Mganga alisema majina hayo yaliingizwa kwenye mnada wa saba kinyume cha sheria, likiwamo jina la mtuhumiwa wa pili ambaye ni rafiki yake Said Ally Tindwa, jina la mdogo wake Abdulatif Hamisi Tewele na mama, Hawa Salum Pange, akidai walikiuzia chama kilo 6,849 za korosho zenye thamani ya Sh. 16,576,836.

Pia alisema katika mnada huo wa saba, Rahim aliingiza jina la mfanyakazi mwenzake, Kuruthumu Hassani Mfaume, ambaye ni mtuhumiwa wa nne, alidaiwa kukiuzia chama hicho kilo 2,995 na kuingiziwa kwenye malipo ya Sh. 7,248,379, wakati sio kweli.

"Utaratibu huu pia ulifanywa katika mnada wa nane kwa kuwaingiza tena watu wale wale kasoro ilikuwa idadi ya kilo na fedha," aliongeza Mganga.

Alifafanua kuwa kutokana na kitendo hicho, watuhumiwa wanakabiliwa na makosa matano, likiwamo la kughushi nyaraka, kuwasilisha nyaraka za uongo, wizi, kusababisha hasara na utakatishaji wa fedha haramu.

Alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani wakati wowote kuanzia sasa, kwani taratibu zote zimekamilika, ikiwamo kupata kibali kutoka ofisi ya mashtaka.

# Shahidi adai kigogo NIDA kulipwa mil. 3/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeambiwa na Meneja wa Bank of Africa (BOA), Tawi la Kariakoo, Fednand Urasa, kwamba mshtakiwa George Ntalima, alilipwa Shilingi milioni tatu na kampuni ya udalali wa bima, Aste Insurance.

Ntalima ambaye ni Ofisa Usafirishaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), anakabiliwa na wenzake wanne akiwamo Mkurugenzi wa zamani, Dickson Maimi, mashtaka 50 ikiwamo kutakatisha Sh. bilioni 1.175.

Urasa alitoa madai hayo jana wakati akitoa ushahidi wa Jamhuri katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Zacharia Ndeskoi, Urasa alionyesha nyaraka ya malipo hayo kupitia taarifa ya mteja (Bank statement) iliyotolewa na benki hiyo Februari 19, 2018.

Shahidi alidai kuwa taarifa hiyo ni ya kati ya Januari mosi, 2012 mpaka Mei 3, 2016 inayoonyesha alitia saini yeye pamoja na meneja Juliety Mwanga.

"Mheshimiwa kwa mujibu wa nyaraka hii inaonyesha Juni 19, 2012, katika akaunti ya kampuni hiyo, iliingia Sh. milioni 31.6 ikitokea NIDA Dar es Salaam, baada ya kampuni hiyo kupokea kiasi hicho cha fedha, Juni 20, 2012, Shilingi milioni tatu zililipwa kwa Ntalima kwa hundi ya benki hiyo," alidai shahidi.

Akifafanua ushahidi wake, alidai kuwa taarifa zote mteja hutunzwa katika mfumo wa benki.

Kesi hiyo imeahirishwa na leo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Meneja Biashara wa NIDA, Aveln Momburi, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond na Xavery Kayombo.

# Kortini tuhuma za kusafirisha vinyonga

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI watatu wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka ya kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na biashara ya nyara za serikali wakiwamo vinyonga.

Washtakiwa hao, Erick Ayo, Alli Ringo na Azizi Ndago, wote ni wakazi wa jijini Dar es Salaam.

Walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, aliyepangiwa kusikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Kija Luzungana, alidai kuwa kati ya Desemba 22, 2020 mahali tofauti ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Pwani, kwa makusudi walishirikiana kuongoza genge la uhalifu na kusafirisha vinyonga wenye thamani ya Sh. 8,546,889 mali ya Serikali ya Tanzania bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori.

Katika shtaka la pili washtakiwa wote kwa pamoja na kwa makusudi wakiwa na nia ya kujipatia faida, kati ya Desemba 22, 2020 na Februari 21, 2021, Mkoa wa Dar es Salaam, Morogoro, Tanga na Pwani, walijihusisha na biashara ya nyara za serikali kwa kusafirisha vinyonga 74 wenye thamani ya fedha zilizotajwa.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo. Imeahirishwa mpaka Februari 29, 2021 itakapotajwa. Washtakiwa walitakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho na kusaini hati ya dhamana ya Shilingi milioni mbili kila mmoja.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe (kushoto), akiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, David Mwakiposa Kihenzile (katikati) na wajumbe wa kamati hiyo, wakikagua utendaji kazi wa kiwanda cha nguo cha Took Garmet, kinachotengeneza nguo aina ya jeans, fulana na kuajiri wafanyakazi zaidi ya 3,700 katika eneo maalum ya uwekezaji kwa mauzo ya nje (EPZA), Ubungo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: ELIUD RWECHUNGURA**

# Lukuvi amaliza mgogoro umiliki ardhi

**Na Munir Shemweta**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemaliza utata uliojitokeza kuhusu mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na mmiliki wa viwanja, Dk. Khalifa Msami katika Mtaa wa Nzasa, Kijitonyama, Dar es Salaam.

Mgogoro huo ulikuwa kati ya wananchi ambao ni wakazi wa mtaa huo na Dk. Msami ambaye ni mmiliki wa viwanja namba 296 na 297 kuhusu umiliki mipaka ya eneo hilo.

Waziri Lukuvi alikwenda katika eneo hilo lililoko barabara ya Segera juzi baada ya kupokea malalamiko kuhusiana na matumizi ya mipaka ya eneo hilo.

Akiwa katika eneo hilo, Lukuvi alibaini ukiukwaji wa mipaka ya maeneo hayo huku baadhi ya wamiliki katika nyumba za mtaa huo wakiongeza ukubwa wa maeneo na kuingia sehemu ya barabarani kwa takriban mita nne na wengine wakiziba mifereji ya majitaka.

Kutokana na hali hiyo, Lukuvi aliagiza ofisi ya ardhi mkoa wa Dar es Salaam pamoja na idara ya ardhi katika Manispaa ya Kinondoni kuhakikisha inafufua mipaka ya maeneo hayo haraka ili kubaini wamiliki waliojiongezea maeneo kinyume cha sheria.

"Uamuzi wangu baada ya kubaini ukiukwaji, timu ya wilaya na mkoa ije ifufue mipaka bila kubomoa nyumba na mjue ni kosa kujiongezea eneo. Ukimilikishwa jenga kwa mpango wa serikali si kujiamulia na heshimu mipaka ya serikali," alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, timu kutoka ofisi hizo mbili itakapokwenda kufufua mipaka katika eneo hilo, itamwonyesha kila mmiliki eneo lake na kusisitiza kuwa baada ya kukamilika kazi hiyo, kila mmiliki wa ardhi atatakiwa kubaki eneo lake kulingana na ukubwa wa kiwanja chake na maeneo ya barabara pamoja na njia za majitaka yaachwe wazi.

"Lakini tumeshajua katika viwanja vyenu kuna walioongeza maeneo kwa madai kuwa ni maeneo ya wazi, msitamani vitu vya watu wengine. Mjenge kwa kuzingatia maeneo yanayowahusu na si vinginevyo," alisema Lukuvi.

Baadhi ya wamiliki wa nyumba katika Mtaa wa Nazasa, walimweleza Waziri kuwa walifanya uamuzi wa kuongeza maeneo bila kujua na kudhani maeneo hayo ni ya wazi na kumwomba kuangalia namna ya kuwasaidia kwa kuwa wameshajenga katika maeneo hayo.

HABARI KITAIFA

# Vijiji vilivyobakia kupata umeme ndani ya miezi 18

**Na Mwandishi Wetu, TABORA**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amezindua mradi wa kitaifa wa usambazaji umeme vijijini, awamu ya tatu, mzunguko wa pili utakaokamilisha usambazaji wa umeme katika vijiji vyote 1,974 vilivyosalia nchini.

Uzinduzi huo ulifanyika katika Kijiji cha Ugaka, wilayani Igunga mkoani Tabora, juzi.

Dk. Kalemani alisema mradi huo utagharimu Sh. trilioni 1.24 za kitanzania na utatekelezwa kwa miezi 18 kuanzia sasa katika mikoa yote.

Waziri Kalemani alisema kila wilaya itakuwa inapewa mkandarasi wake kutekeleza mradi huo ili kukamilisha kazi hiyo kwa wakati, tofauti na ilivyokuwa katika miradi iliyotangulia, ambapo mkandarasi alikuwa akipewa zaidi ya mkoa mmoja kufanya kazi hiyo, jambo ambalo lilichangia kusuasua na kutokamilika kwa wakati kwa mradi.

Alisema kwa mantiki hiyo, hakuna kuongeza muda wa ziada kwa mkandarasi yeyote atayeshindwa ama kuchelewa kukamilisha mradi huo kwa muda uliopangwa, na atayeshindwa kukamilisha mradi huo kama mkataba unavyoelekeza, atafutiwa mkataba wake na kufikishwa mahakamani.

"Kwa sasa hakuna kuongeza muda kwa mkandarasi yeyote atayecheleweshwa mradi, tutachukuwa hatua za kisheria kwa mujibu wa mkataba, ikiwamo kufuta mkataba wa mkandarasi na kumfikisha mahakamani, tumeamua kutoa mkandarasi mmoja kwa kila wilaya, hii yote ni kuhakikisha kazi hii inakamilika kwa wakati ndani ya miezi 18, tutakuwa tumemaliza kusambaza umeme katika vijiji vyote 1,974 vilivyosalia nchi nzima," alisema Dk. Kalemani.

Aliendelea kuwasisitiza wananchi kulipia gharama ya Sh. 27,000 tu katika vijiji na mitaa, na kamwe wasikubali kurubuniwa maofisa wasio waaminifu pamoja na vishoka watakaotaka kuwatoza gharama kubwa zaidi.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, aliwataka wawekezaji kwenda kuwekeza katika mkoa huo, kwa kuwa una fursa nyingi za uwekezaji kutokana na shughuli mbalimbali za kilimo, ufugaji pamoja na uchimbaji madini na kwamba kuna umeme wa kutosha.

## Bunge lakunwa ujenzi wa nyumba Magomeni

**Na halfani Chusi**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba za Magomeni mkoani Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Seleman Kakoso, alibainisha kuridhishwa kwao na mradi huo jana kamati hiyo ilipozuru kukagua maendeleo ya mradi huo.

Alisema mradi umekwenda vizuri na kwamba Sh. bilioni 50 zilizopitishwa kuugharamia, zimetendewa haki.

"Ukiangalia jinsi mahali hapa palivyo, ukaambiwa mradi huu umegharimu Sh. bilioni 50, siyo rahisi kuamini lakini hii yote ni kwa sababu TBA (Wakala wa Majengo) wameonyesha ubunifu wa hali ya juu sambamba na kutengeneza mitambo ya kutengeneza malighafi za ujenzi humu humu ndani.

"Kama ambavyo tumepita na tumeona mtambo wa kutengeneza matofali na kuchakata zege. Hayo yote yamesababisha gharama kupungua kwa kiasi kikubwa.

"Ilishazoeleka kwamba miradi hii ya ujenzi kwa mainjinia walio wengi ni ya kupigia pesa, lakini hilo limekuwa kinyume kwa TBA," alisifu.

Kakoso aliiomba serikali kulipa madeni inayodaiwa na TBA na kuwapa kipaumbele baadhi ya wafanyakazi waliokuwa wanafanya kazi kwa kujitolea huku wakiwa na sifa za kuajiriwa.

"Nitoe ombi kwa serikali kuwalipa pesa zao wafanyakazi wa TBA, ili waweze kuongeza motisha na morali zaidi ya kufanya kazi.

"Naibu waziri hilo lisimamie hawa watu wapate staiki zao. TBA wamejenga majengo ya Mji mpya wa serikali pale Dodoma lakini hawajalipwa.

"Muwape kipaumbele cha nafasi za ajira hasa wale ambao walikuwa wanajitolea ilhali wana sifa za kuajiriwa," alishauri.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema mradi huo unatarajiwa kukabidhiwa mwezi ujao.

"Ninamshukuru Rais (John) Magufuli kwa mawazo yake na kuamua kuukabidhi mradi huu kwa TBA na hatimaye leo hii upo ukingoni na tunatarajia kuukabidhi kwa walengwa mwezi wa nne (Aprili) mwishoni kama ilivyopangwa," alisema.



Katibu wa Afya Mkoa wa Dar es Salaam, Sister Mathew, akimsaidia mtoto Halima Juma kutoka Zanzibar, kuingia ukumbini wakati wa semina kwa waandishi wa habari, kuhusu uandishi wa habari za lishe bora, iliyoandaliwa na Chama cha Wazazi wa Watoto wenye Ulemavu wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi Tanzania (ASBAHT), kwa kushirikiana na Asasi ya Child Help Tanzania na ASBAHT Zanzibar, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Marekani yamwaga bilioni 18.5/- chakula wakimbizi

**Na Mwandishi wetu**

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) imetoa Dola za Marekani milioni nane (sawa na Sh. bilioni 18.5) kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kwa ajili ya msaada wa chakula kwa wakimbizi.

Kati ya fedha hizo, Dola milioni sita (Sh. bilioni 13.9) zitanunua chakula kwa wakulima wa ndani na Dola Milioni mbili (Sh. 4.6) zitanunua mbaazi za manjano kwa ajili ya kusaidia kukuza uchumi wa nchi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Ubalozi wa Marekani nchini, makabidhiano ya msaada huo yalifanyika katika Bandari ya Dar es Salaam na kwamba msaada huo ni kwa ajili ya kambi za wakimbizi za Nduta, Mtendeli na Nyarugusu.

"Tunapenda kuishukuru serikali ya Marekani kwa ukarimu wanaoonyesha na kuendelea kutoa msaada. Msaada huu umetimiza ahadi yao ya kuendelea kuwasaidia takribani wakimbizi 220,000 wa Burundi na Congo ambao wanategemea sana msaada wa chakula kutoka WFP," alisema Sarah Gibson, Mwakilishi wa WFP Tanzania.

"Sehemu ya msaada huo hutumiwa kununua chakula kutoka kwa wakulima wadogo nchini Tanzania. Hii inaonyesha uwekezaji mzuri katika uchumi wa ndani," alibainisha.

Naye Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald Wright, alikabidhi msaada huo na kusema USAID itatoa msaada wa chakula cha dharura kwa wakimbizi na watafuta hifadhi wanaokaa katika kambi na kwamba msaada huo utajumuisha upatikanaji wa bidhaa ndani ya nchi kwa njia ya kujitolea.

"Mchango huu umetokana na ukarimu wa watu wa Marekani, na tunajivunia matokeo yatokanayo na kuokoa maisha katika jamii zilizo hatarini. Serikali ya Marekani inaunga mkono ulinzi wa wakimbizi, wanaotafuta hifadhi, waathirika wa migogoro, watu wasio maeneo, na wahamiaji walio katika mazingira hatarishi Tanzania na duniani kote," alisema.

"Tunatambua juhudi za muda mrefu za Tanzania kama nchi mwenyeji kwa wakimbizi na wanaotafuta hifadhi na tunahimiza sana serikali ya Tanzania kuhakikisha mahitaji ya kibinadamu ya wahamiaji wote walio katika mazingira magumu nchini Tanzania yanatimizwa," aliongeza.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Makazi na Makambi katika Idara ya Huduma za Wakimbizi, Nsato Msanzya, Wizara ya Mambo ya Ndani na Mkurugenzi wa Bandari, Elihuruma Lema.

WFP husambaza mgawo kwa kila mwezi unaojumuisha nafaka, kunde, chumvi, mafuta ya kupikia na chakula cha mahindi chenye viini lishe, pamoja na vyakula maalum vyenye lishe kwa wajawazito, wanawake wanaonyonyesha na watoto chini ya miaka mitano.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Polisi sasa lijisafishe dhidi ya matukio haya

**WAJIBU** wa Jeshi la Polisi kisheria ni kulinda raia na mali zao, kwa kuhakikisha wanatenda haki na inaonekana kutendeka, inapokuwa kinyume inaleta ukakasi na kupunguza imani ya raia kwao.

Katika operesheni ya kukamata nyama za mafungu nje ya machinjio ya Vingunguti jijini Dar es Salaam, iliyofanywa kwa ushirikiano kati ya jeshi hilo na Bodi ya Nyama, yameibuka malalamiko ya namna raia walivyoporwa nyama na baadhi ya askari polisi kugawana ndani ya jengo la upelelezi. Walidai nyama hiyo zaidi ya kilo 800, ilichukuliwa na askari ambao waligawana, huku kila aliyehoji aliwekwa ndani na kutishiwa kuchukuliwa hatua zaidi.

Katika video ya mmoja wa waathirika wa operesheni hiyo katika kikao cha pamoja baina ya jeshi hilo, ofisi ya mbunge, Bodi ya Nyama na Jiji yaliibuka madai mazito dhidi ya polisi Buguruni kugawana nyama waliyokamata, huku wakiwaambia wananchi kuwa iliteketezwa.

Wafanyabiashara hao waliibua madai mazito kuwa polisi waliingia kwenye mabucha na machinjio na kubeba nyama kisha kutoweka nayo, na walivyofika kituo cha polisi kudai haki yao, waliswekwa ndani, kulipishwa faini ya kuanzia Sh. 100,000 na hawakupata nyama.

Mmoja alieleza walivyomkamata ndani ya bucha na walimtaka kulipa faini, alivyowahi kituoni ili alipe faini akakuta askari wenye visu wakigawana nyama na kutumia pikipiki kuiondoa kituoni na alipohoji alikamatwa na kuwekwa ndani.

Walieleza kwa uchungu hasara waliyoipata na fedha za mtaji ni za mkopo huku mmoja akieleza kupoteza Sh. 706,000, huku wakipinga madai kuwa nyama ilikamatiwa nje ya machinjio, kwamba ni uongo kwa kuwa ilikamatiwa ndani ya machinjio.

Madai haya siyo ya kupuuza wala kuchukulia kwa wepesi kwa kuwa yanashusha hadhi na imani ya raia dhidi ya jeshi hilo, tunatarajia kuona hatua madhubuti za kulisafisha jeshi hilo kuchukuliwa.

Kumekuwa na madai ya kukosekana uaminifu kwa baadhi ya askari polisi wasioheshimu maadili ya kazi yao ambao kwa makusudu anaumiza raia kwa kupora mali zao, na wanapojaribu kudai haki wanaishia kubambikiwa kesi.

Pia yamekuwapo madai ya kupotea au kuibwa kwa baadhi ya vidhibiti vya ushahidi katika kesi mbalimbali kama magari kutolewa vifaa muhimu yanapokuwa polisi, na iwapo raia akisimama kudai haki yake awe na uhakika wa kubambikiwa kesi.

Hali hii ikiachwa hivi maana yake ni kuongeza idadi ya watu wenye kesi za kubambikiwa na wenye mamlaka. Ni muhimu sana jeshi hilo likatoka hadharani na kujisafisha dhidi ya haya yote, vinginevyo watapoteza imani kwa kuwa wanajenga na kuendeleza chuki, uchungu na kisasi kwa raia ambao watashindwa kushirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu yao.

Tunatarajia kusikia hatua zimechukuliwa kwa wahusika, tunahitaji kuona uwajikaji wa wote waliohusika. Tunapata imani hiyo baada ya taarifa kuwa Mkurugenzi wa Upelekezi wa Makosa ya Jinai (DCU) ameanza uchunguzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hii hapa kinga inayoepusha migogoro ya kugombea mirathi katika familia

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya mambo yanayowakumba baadhi ya wanawake mara tu wanapofiwa na waume zao, ni kufanyiwa vurugu, ubaguzi, unyanyapaa na wakati mwingine kuporana mali.

Ni hatua inayosababisha watu kupoteza haki zao baada ya waume, wake au wazazi na hata mtoto kufariki, pasipo kuacha wosia. Hivyo, wanaziacha familia katika mazingira magumu, yakiwamo ya kugombea mali.

Inaelezwa kwamba, hali hiyo hutokea ama kwa marehemu kutojua au kwa kujua. Mara nyingi mhusika aliyeaga dunia anapoacha kuandika huo wosia, mwisho wa siku hilo huangukia migogoro kwenye familia hadi kufikia hatua wanafamilia wanasambaratika, kutoka muungano wa awali.

Katika kuhakikisha wanaondokana na tatizo hilo, serikali kwa kushirikiana na taasisi zake na wadau wengine, imekuwa ikijitahidi kumsaidia kila Mtanzania aelewe umuhimu wa kuandika wosia, unaosaidia kuacha maelekezo wakati yeye hayupo duniani.

Serikali inafanya hivyo kwa kutambua kila binadamu yupo safarini kuelekea kifo katika tarehe asiyoijua, jambo linalolazimisha wajibu wa kuandikiwa wosia ndani ya uhai, ili anapokufa anakuwa katika hatua ameepusha migogoro mingi.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Dovetha Kamuzora, kuna wakati alilieleza hilo, kwamba katika elimu yake kwa baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, akiwa na msisitizo unaodai kuwapo wasimamizi wa mirathi wanaoaminika.

Anachohimiza ni kwamba, watu waachane na dhana kwamba kuandika wosia ni uchulo, bali wafanye hivyo kwa kutambua kuwa ni njia sahihi ya kuiacha familia yake nje ya migogoro kati yao au na ndugu.

Kimsingi, ushauri wa Msajili Mahakama unahimiza suala muhimu kwa Watanzania wote wabadilike wakizingatia imani ya kijamii ya kuandika wosia pale wanapofariki, ili wasiache migogoro nyuma

**Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Dovetha Kamuzora, kuna wakati alilieleza hilo, kwamba katika elimu yake kwa baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, akiwa na msisitizo unaodai kuwapo wasimamizi wa mirathi wanaoaminika.**

inayosambaratisha familia kwa jumla.

Ieleweke, msimamizi mirathi daima huwa ni mteule mwaminifu, kwa kuwa wapo baadhi huteuliwa kwa wajibu huo kifamilia, badala wanageuka kuwa tatizo kubwa.

Hapo kunatupatia masomo ya kuzingatia, ili kutoa majawabu sahihi ya kuepusha migogoro pale mmoja wa wenza au mzazi anapofariki dunia. Wosia unatoa majibu inayofunga mijadala isiyokuwa na tija kuhusu mirathi, chini ya msimamizi anayeaminika.

Kwa kuwa kila mmoja wetu ni marehemu mtarajiwa, suala la kuzingatia maelekezo yanayoandikwa ndani ya wosia, linahusu kila mmoja ambaye anaguswa na andiko hilo.

Zipo taratibu za uandishi wa wosia kisheria, zikiwamo kufanyiwa ushuhuda wa watu wengine na kuna taratibu zinazoenda mbali, kwamba asiyejua au hawezi kusoma na kuandika, naye amewekewa utaratibu maalum.

Kwa ujumla, wosia wa maandishi haubadilishwi na wosia wa mdomo, ila wa mdomo unaweza kubadilishwa na wa maandishi, na mtoa wosia ana haki ya kuandika au kutaja sehemu tu ya mali zake katika wosia wake.

Huwa kuna mengi, ikiwamo vigezo vya kisheria, kwamba inapogundulika katika uandishi mhusika akili yake haikuwa timamu kwa namna yoyote, moja kwa moja inageuka kuwa batili.

Kiserikali, mamlaka yenye dhamana na utunzaji wa wosia, Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) umeweka wazi namna mtu anaweza kuandika na kwenda kuutunza huko kwa ajili ya usalama zaidi.

Ikumbukwe kuwa, RITA ni chombo cha serikali chenye dhamana ya kusimamia mirathi na utunzaji wosia ni sehemu ya majukumu yake, hivyo mwandikaji anapokosa mbadala wa kupatunza salama, basi chombo hicho cha serikali kinabeba wajibu.

# Wataalamu wa ndani wapigiwa debe utafiti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Prof. Siza Tumbo, ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushiriki Tanzania (TCDC) na vyama vya ushirika kufanya utafiti ili kutafuta suluhu ya matatizo katika sekta hiyo.

Pia amevitaka vyama vya ushirika kutenga fedha kwa ajili ya kuwezesha wataalamu mbalimbali kufanya utafiti huo na kuacha kutegemea wafadhili kutoka nje ya nchi.

Prof. Tumbo aliyasema hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akifungua kongamano la utafiti wa ushirika litakalofanyika kwa siku tatu.

Alisema upo umuhimu wa kufanyika kwa utafiti unaohusu sekta hiyo ya ushirika ili kusaidia kutatua matatizo yaliyomo na kuyapatia majibu.

"Lazima tuwekeze katika utafiti mbalimbali ambao unaweza kutatua changamoto zilizopo kwenye ushirika nchini ili kuweza kupiga hatua kitaifa na kwa mtu mmoja mmoja," alisema Prof. Tumbo.

Pia alisema ipo haja kwa vyama vya ushirika nchini kuwekeza fedha kwenye utafiti ili kuwasaidia watafiti wa ndani.

"Mnatakiwa kutenga fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti katika sekta ya ushirika kwani kama wataalamu wetu watakosa fedha na kwenda kupata kwa wafadhili nje ya nchi basi fedha zile zinakuwa na masharti mengi," alisema.

Alisema fedha za wafadhili kwa ajili ya utafiti hazitakuwa na msaada kutokana na masharti wanayotakiwa kuyatekeleza watafiti wakati mwingine hayajibu maswali ya matatizo yaliyopo katika ushirika.

Kadhalika, aliagiza kwa wataalamu wote wanaofanya utafiti katika sekta hiyo kuandaliwa kwa lugha ya Kiswahili ili uweze kutumika kwa vyama vyote vya ushirika.

Naye Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Dk. Benson Ndiege, alisema katika kongamano hilo watafiti kutoka vyuo na taasisi watawasilisha matokeo yake ikiwa ni pamoja na wadau wa maendeleo ya ushirika wanaofanya kazi na vyama vya ushirika kwa kuangalia fursa, changamoto na mapendekezo yake.



Mwendesha guta akiwa amebeba geti la chuma na abiria juu, katika eneo la Kigogo, jijini Dar es Salam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC arejesha ardhi ya mwekezaji kwa kijiji

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Marco Gaguti, ameagiza ardhi iliyochukuliwa na mfugaji Athuman Makoye katika eneo la Rusumo wilayani Ngara kurejeshwa katika mamlaka ya serikali ya kijiji.

Alitoa agizo hilo alipokuwa katika ziara, baada ya kufika eneo la Rusumo lenye mgogoro kati ya Makoye na wananchi, kwa madai kuwa mfugaji huyo anawazuia kuingiza mifugo katika eneo hilo la kijiji.

"Tunamruhusu mtu huyu awe sehemu ya jamii yetu, lakini asipore na kujimilikisha ardhi, kwa hiyo Makoye umejimilikisha ardhi kwa sababu ya viongozi wenye dhamira mbaya," alisema Brigedia Jenerali Gaguti.

Baada ya majibizano yaliyodumu kwa muda mfupi, Gaguti aliagiza mfugaji kuwekwa chini ya ulinzi, huku akitoa maagizo juu ya ardhi hiyo na kusema kuwa hakuna mtu yeyote anayeruhusiwi kuweka uzio kwenye eneo hilo la kijiji, kwa kuwa uongozi wa kijiji una ukomo wake wa mamlaka katika suala la umiliki wa ardhi.

Pia aliagiza vyombo husika ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza suala hilo na kuwachukulia hatua wote waliohusika katika kumpatia ardhi mwekezaji huyo kinyume cha utaratibu wa kisheria wa umiliki wa ardhi.

"Ardhi yote ya kijiji itarejeshwa kwenye mamlaka na miliki ya wananchi wenyewe na wale wote ambao wapo humu kinyemela lazima watafute uelekeo au wakaombe upya kwa wananchi wawajadili kama wana haki ya kuendelea kuishi hapa," alisema Gaguti.

Awali akijitetea mbele ya Gaguti, mwekezaji huyo alisema ardhi hiyo alipewa na uongozi wa kijiji, baada ya kupewa sharti la kujenga vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Ngoma na yeye kutekeleza sharti hilo.

"Nilifika katika uongozi wa kijiji nikaomba eneo la kuchungia, baada ya kuomba nilipewa masharti ya kwamba wewe utatufanyia nini, nikawaambia naomba mnipe kitu mnachotaka nifanye wakaniambia nijenge shule nikajenga shule hapo Ngoma wakati huo shule hiyo haikuwapo, tukakubaliana nijenge madarasa mawili na nikatekeleza," alisema Makoye.

Pamoja na maelezo hayo, Gaguti alisema haikuwa sahihi kwa mwekezaji huyo kupewa ardhi yote ya kijiji kwa kuwa ukomo wa serikali ya kijiji katika kutoa ardhi ni hekari 50.

# Elimu rushwa ngono sasa shule kwa shule

**Na Halfani Chusi**

TAASISI isiyo ya kiserikali inayojihusisha na utetezi wa wanawake katika jitihada za maendeleo (WAJIKI), imeendelea kutoa elimu kuhusu rushwa ya ngono na unyanyasaji wa kijinsia shule kwa shule.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Janeth Mawinza, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, alipotembelea shule ya tatu wilayani Kinondoni kwa lengo la kutoa elimu hiyo.

Alisema mwanamke hasa mwanafunzi, hawezi kufikia malengo yake kielimu bila kupambana na vikwazo vya ukatili wa kijinsia na rushwa ya ngono.

"Tunawashukuru Women Fund Tanzania (WFT), kwa kutufadhili katika huu mradi. Kwa kifupi, tulianza kutoa elimu hii mtaa kwa mtaa na kufanya maandamano ya kupiga vita rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia.

"Sasa tumeona tupite shuleni ili tuifikishe elimu hii kwa wanafunzi wa kike ambao ndiyo waathirika zaidi, ili wajue namna ya kupambana na changamoto hizo pindi wanapokutana nazo," alisema.

Mawinza alisema kuwa kwa miaka mingi suala la rushwa ya ngono limekuwa likifumbiwa macho, akifafanua kuwa halizungumziwi kama rushwa nyingine zinavyozungumziwa.

Alisema kwa kutambua mwanamke ni chachu ya maendeleo, wameamua kuifikisha elimu hiyo mpaka shuleni ili kupata kizazi chenye usawa.

Mawinza alizitaja shule ambazo wameshazifikia na kutoa elimu ni pamoja na Shule ya Msingi Msisili B iliyoko Mwananyamala, Shule ya Msingi Mivumoni (Wazo) na Shule ya Sekondari Twiga (Wazo).

Aliyataja madhara rushwa ya ngono kwa mwanafunzi kuwa yanajumuisha kuathirika kisaikolojia, mimba za utotoni, kupata magonjwa ya zinaa na kukatisha malengo na ndoto za watoto wa kike.

Mwalimu wa Jinsia katika Shule ya Sekondari Twiga, Nyasati Mwisira, alisifu kutolewa kwa elimu hiyo kwa wanafunzi na walimu ili kuongeza uelewa.

"Sisi walimu kupitia darasa la leo, tumejifunza mengi sana kuhusu masuala ya rushwa ya ngono na ukatili wa kijinsia, lakini kubwa zaidi tumejua sehemu sahihi ya kufikisha taarifa za mtoto anapofanyiwa ukatili na zikashughulikiwa bila tatizo," alisema.

# Mapendekezo bajeti mkoa Pwani bil. 298/-

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KAMATI ya Ushauri ya Mkoa (RCC) wa Pwani, imepitisha mapendekezo ya mpango na bajeti wa Sh. bilioni 298.5 kwa mwaka 2021/22. Rasimu hiyo ya bajeti ni ongezeko la asilimia 9.38 kulinganisha na bajeti ya mwaka 2020/21.

Aliwasilisha mapendekezo hayo katika kikao cha kamati hiyo kilichofanyika jana mjini hapa, Mchumi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Gerald Mbosori, alisema utekelezaji wa mpango na bajeti utaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya miaka mitano.

Mbosori alisema vipaumbele vya mkoa huo kwa mwaka 2021/22 ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya elimu na afya, kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani na uandaaji wa mazingira wezeshi ya uwekezaji na ujenzi wa viwanda.

Mchumi huyo alisema kwa mwaka 2020/21, mkoa uliidhinishiwa matumizi ya Sh. bilioni 272.9 na hadi Desemba, mwaka jana, sekretarieti ya mkoa ilikusanya maduhuli ya Sh. bilioni 3.7 sawa na asilimia 6.12.

Pia alisema katika kipindi hicho, halmashauri zote za mkoa zikikusanya Sh. bilioni 16.6 sawa na asilimia 43.04 ya malengo yaliyowekwa.

Alisema ufinyu wa makusanyo hayo ulitokana na vikwazo vinavyosababisha baadhi ya halmashauri kutofikia malengo ikiwa ni pamoja na wigo mdogo wa vyanzo vya mapato.

Vikwazo vingine, kwa mujibu wa Mbosorim ni usimamizi usioridhisha kwa baadhi ya vyanzo kama leseni za biashara, vileo na ushuru wa nyumba za kulala na upungufu wa vitendea kazi kama magari na pikipiki kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji. Akifunga kikao hicho ambacho kilipitisha mapendekezo hayo kwa kupiga kura, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alizitaka halmashauri kuhakikisha zinasimamia na kubuni vyanzo vipya vya mapato ya ndani.

Ndikilo alisema uwepo wa vyanzo vya mapato vya ndani unasaidia kufanya miradi ya maendeleo kwa wakati bila kusubiri fedha kutokana serikali kuu. Pia aliwasisitiza wataalamu katika sekretarieti ya mkoa na halmashauri kuwa makini na kujenga uaminifu katika ukusanyaji wa mapato.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo (kushoto) na Wajumbe wa Kamati hiyo, wakimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (kulia), walipotembelea chumba cha kisasa cha upasuaji katika jengo jipya la huduma ya afya ya mama na mtoto, hospitalini hapo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Atoweka nyumbani kwa wazazi wake

**Na Mwandishi Wetu**

SAMSON Kiduko (42), anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao tangu Machi 3, mwaka huu.

Baba mzazi wa Samson, Alphonce Kiduko, akizungumza na Nipashe jana, alisema siku hiyo hadi sasa pamoja na kumtafuta katika maeneo tofauti ikiwamo kwa ndugu, jamaa na marafiki, hajulikani alipo kijana wake.

Siku hiyo, kwa mujibu wa Mzee Kiduko, Samson aliwaaga zazazi wake nyumbani kwao, Tabata Segerea, kuwa anakwenda kwenye shughuli zake na kuahidi kwamba atarejea jioni lakini haikuwa hivyo.

Alisema awali alikuwa akifanya shughuli zake mkoani Arusha, kabla ya mwaka huu kuhamia Dar es Salaam alikopata kazi kwenye kampuni ya uhamasishaji biashara.

"Tumemtafuta kote, Polisi tumeripoti jana (juzi). Tumeenda hadi hospitali na marafiki zake lakini haijajulikana alipo hadi leo (jana)," alisema Kiduko.

Pia alisema kutokana na kutokujulikana alipo, walitoa taarifa katika Kituo cha Polisi Kinyerezi na kupewa jalada lenye namba KINY/RB/258/2021 na kuendelea juhudi za kumtafuta.

Mzee Kiduko aliomba yeyote atakayemwona atoe taarifa kupitia namba **0754 372 4544** na **0657 137 000.**

# JKT yajitosa kuboresha zao la kahawa

**Na Renatha Msungu,** MBEYA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), linakusudia kuinua uzalishaji wa kahawa katika vikosi vyake vitano, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la serikali la kuongeza mapato ya fedha za kigeni.

Imebainishwa kuwa tayari jeshi hilo limepokea kilo 300 za mbegu za kahawa kutoka Bodi ya Kahawa ambazo zitazalisha miche milioni moja kwa lengo la kuigawa kwa wananchi na itakayobaki, itatumiwa na vikosi kuendeleza mikakati ya kuinua zao hilo.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Charles Mbuge, alibainisha hayo katika ziara yake kwenye Kikosi cha 844 JKT Itende kilichoko mkoani Mbeya, ambacho huzalisha kahawa na mazao mengine ya chakula na biashara.

Meja Jenerali Mbuge alivitaja vikosi vingine ambavyo vinazalisha zao hilo kuwa ni JKT Ruvuma, Kigoma, Mara na Mlale Ruvuma.

"Tunazalisha mazao ya kimkakati lengo likiwa ni kuongeza uchumi wa taifa kupitia fedha za kigeni zinazotokana na mazao hayo," alisema.

Akizungumzia mbegu zilizotolewa na Bodi ya Kahawa, kiongozi huyo wa jeshi alisema ni utekelezaji wa malengo ya mkataba wa kuendeleza zao hilo katika Kikosi cha JKT Itende na vikosi vingine.

Meja Jenerali Mbuge alisema wamejipanga kuboresha mazao ya kimkakati ikiwamo kahawa ili kusaidia kukuza uchumi wa taifa.

"JKT tunatekeleza agizo la Rais, Dk. John Magufuli la kutaka tujitegemee katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, ili kuepuka kutegemea fedha za serikali," alisema.

Ili kufanikisha hilo, alisema jeshi hilo limeweka mikakati ya kuhakikisha linaongeza uzalishaji kwenye mazao ya kilimo na biashara.

Kaimu Mkuu wa Utawala JKT na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo cha Mkakati, Kanali Hassani Mabena, alisema serikali imeweka mkakati kuhakikisha mazao ya kimkakati yanazalishwa, hivyo jeshi hilo huzalisha mazao yanayokwenda kutoa malighafi za viwanda.

Meneja wa Shamba wa Kikosi cha JKT Itende, Kapteni Emmanuel Mwakimage, alisema kikosi hicho kwa sasa kinaondoa miche ya zamani ya kahawa na kupanda miche mipya yenye ubora.

Alisema kikosi kimeanza kwa kupanda ekari 50 miche mipya ambayo huanza kutoa matunda baada

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yaokoa mil.15/- za mstaafu

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Kagera imeokoa na kukabidhi Sh. milioni 44.8 zitokanazo na mikopo umiza, ubadhirifu na utoaji wa stakabadhi feki.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Kagera, John Joseph, alitoa taarifa hiyo alipozungumza na wandishi wa habari.

Alisema wamefanikiwa kurudisha Sh. milioni 15 za mstaafu wa utumishi wa Halmashauri ya Muleba, ambaye alikuwa ofisa biashara, Laurianian Rweyemamu.

"Mstaafu huyu aliingia makubaliano na Daicola Charles, kwa kuchukua fedha kwa mkopo wa Shilingi milioni saba kwa ajili ya kulipia ada za shule za watoto wake, kwa makubaliano ya kurejesha Sh. milioni 14 na kukabidhi kadi ya kutolea fedha (ATM)," alisema Joseph.

"Tulifuatilia zaidi na tulibaini baada ya Laurian kupata fedha za kustaafu Sh. milioni 42, alimfuata Daicola Charles ili ampatie kadi yake ya benki kwa ajili ya kufanya marejesho waliokubaliana, ndipo Laurian alipomwambia kwamba kiasi alichotakiwa kurejesha ni Sh. milioni 40," alisema Joseph.

Pia, alisema kiwanda cha kusindika kahawa cha TANICA, mwaka 2018/2019 kilinunua kahawa kilo 123,570 kwa bei ya Sh. 3,000 kwa kilo moja badala ya Sh. 2,740 kwa mujibu wa soko la kahawa kwenye kampuni ya Arab globe international iliyopo wilayani Ngara, mkoani Kagera.Alisema kahawa hiyo ilizalishwa msimu wa mwaka 2017/2018 na kampuni hiyo ilijipatia manufaa yasiyo halali ya Sh. milioni 29.6.

Aidha, alisema baada ya kufanya mahojiano uongozi wa kiwanda hicho, ulikiri kosa hilo na kuomba kurejesha jumla ya Sh. milioni 26.8 ambazo ni mali ya kiwanda TANICA.Kwa upande mwingine, alisema utoaji wa risiti ya bei ya chini kuliko halisi iliyouzwa bidhaa, taasisi hiyo imeokoa Shilingi milioni tatu kutoka kwenye duka linalouza vinywaji mbalimbali.

Alisema kuwa mmiliki wa duka hilo amekuwa akiandika bei pungufu katika stakabadhi kwa wateja wanaponunua vinywaji.

"Mnano Januari 23, mwaka huu, duka hilo liliuza Whisky ambayo huuzwa kwa gharama ya Sh. 35,000, lakini alitoa stakabadhi inayoonyesha kuwa ameuza kwa bei ya Sh. 3,500 kwa chupa moja," alisema.



Mafundi wa kampuni ya CCECC, wakiendelea na ujenzi wa kituo cha maegesho ya magari cha Manispaa ya Temeke, eneo la makaburi ya Wailes Chang'ombe, mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Vitambulisho vyenye picha kutolewa kwa wamachinga

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

VITAMBULISHO vipya 84,000 vya wamachinga na watoa huduma wadogo vyenye picha vinatarajiwa kutolewa mkoani Mwanza kuanzia sasa hadi kufikia mwezi Julai, mwaka huu.

Mfumo uliowekwa mwaka huu wa ugawaji wa vitambulisho utasimamiwa na Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) na taarifa zote muhimu za kila mfanyabiashara mdogo zitasajiliwa kwenye mfumo kama ilivyo kwa leseni za udereva.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alipokea vitambulisho hivyo na kuvigawa kwa Wilaya za Nyamagana na Jiji la Mwanza, ambayo imepewa 23,000, Ilemela (20,500), Ukerewe (5,500) na Halmashauri za Wilaya za Buchosa, Sengerema, Magu, Misungwi na Kwimba zikipewa kila moja vitambulisho 7,000.

Alisema vitambulisho hivyo vyenye picha vitaanza kuuzwa katika maeneo mbalimbali na kuwataka wakuu wa wilaya zote kuhakikisha vitambulisho hivyo vinatolewa kwa wahusika.Alisema utaratibu huo ulianzishwa na Rais John Magufuli ili kuwasaidia wafanyabiashara wadogo.

"Mlitarajia kukutana na maboksi ya vitambulisho hapa, lakini mfumo umebadilika sasa utatumia simu janja kupata kitambulisho kama ulivyo kwa leseni za udereva," alisema Mongella.

Alisema mfumo huo unalenga kujenga uwezo wa wananchi, utambuzi wa matatizo ya wafanyabiashara hao na jinsi ya kuwasaidia kukuza uchumi wao, wa mkoa na nchi.

## Matatani madai ya kuwazushia uongo viongozi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JESHI la Polisi mkoa Kilimanjaro, linawashikilia watu wawili, Peter Silayo (30) na Melchiory Shayo (36), kwa tuhuma za kusambaza mitandaoni taarifa zisizo na ukweli kwamba baadhi ya kiongozi wakuu wa serikalini ni wagonjwa.

Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Ronald Makona, alisema watuhumiwa hao wa makosa ya kimtandao walikamatwa jana kwa nyakati tofauti.

Silayo ambaye ni mkazi wa Tegeta mkoani Dar es Salaam, alikamatwa katika eneo la Kibaoni, Tarakea, Wilaya ya Rombo na Shayo, ambaye ni mkazi wa Keni, wilayani humo alikamtwa katika Wilaya ya Moshi.

Kamanda Makona alionya wakazi wa Kilimanjaro kuacha kusambaza taarifa zinazoweza kuzua taharuki hasa afya ya mtu mwingine.

"Wote hawa wanakabiliwa na makosa ya kimtandao, kwa kusambaza taarifa za uzushi kwenye mitandao ya kijamii, kinyume na sheria, kuwa viongozi wakuu wa serikali ni wagonjwa.

"Tunawahoji kwa sasa na tukikamilisha taratibu za kipelelezi, watuhumiwa watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili."

Aidha, Kamanda Makona alisisitiza: "Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa mtu yeyote atakayebainika ametoa/amesambaza taarifa za kupotosha umma na kusababisha taharuki kwa jamii."

## DC akataza kukamata wachimbaji wadogo

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKUU wa Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu, Festo Kiswaga, amewapiga marufuku wahasibu wawili kutoka ofisi ya madini ya Mkoa wa Simiyu wanaolalamikiwa na wachimbaji wadogo waliopo mgodi wa Bulumbaka namba mbili kutofika eneo hilo mpaka taratibu za kiuchunguzi zitakapokamilika.

Kiswaga alitoa uamuzi huo jana baada ya kusikiliza kero za wachimbaji wa mgodi huo ambao wamedai wanatoa pesa bila kupewa stakabadhi za kielektroniki pamoja na kuombwa kiasi cha Sh. 500,000 ili wasikamatwe.

" Kuanzia leo sitaki wahasibu hawa wakanyage hapa na ni marufuku kukamata watu hovyo kwenye eneo la mgodi, hakuna mtu mwenye mamlaka ya kukamata wachimbaji wadogo bila sababu kwa kuwa wamekuwa wakionewa na wanaokamatwa ni wanyonge, matajiri hakuna... kabla ya kuwakamata awepo OCD na mtu wa TAKUKURU na chunguzeni Sh. 500,000 waliokuwa wanaombwa wachimbaji wadogo ili sheria ichukue mkondo wake," alisema Kiswaga.

# Vifo vya mama, mtoto vyapungua Kilombero

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

IDADI ya vifo vya kinamama na watoto wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro, imetajwa kupungua kwa zaidi ya asilimia 80 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Sababu imetajwa ni utekelezaji wa mradi wa huduma mkoba wa kliniki inayotembea unaotekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Plan International Tanzania.

Hayo yalibainishwa juzi na mratibu wa chanjo wa Halmashauri ya Mlimba, Nendaheli Malugu, wakati wa ziara ya viongozi wa serikali na shirika hilo kutathmini maendeleo ya mradi huo wa gari maalum la wagonjwa na pikipiki 18 zilizokuwa zimetolewa kwa wahudumu wa afya.

Alisema licha ya Halmashauri ya Mlimba kukabiliwa na upungufu wa zahanati zaidi ya asilimia 67 na uwapo wa vituo vya afya viwili katika kata 16 katika halmashauri hiyo, mradi huo wa huduma mkoba umefika vijiji 117 ambapo kati ya hivyo vituo 36 zinasaidiwa na shirika kwa kuwa ni vigumu kufikika kiraisi.

"Kuanzishwa kwa huduma hii ya mkoba kumesaidia sana kinamama kutembea umbali mrefu kufuata huduma za chanjo, ambapo wakati wa masika hulazimika kutumia gharama kubwa hadi Sh. 30,000 kwa pikipiki kwa umbali wa kilomita 40 kila mwezi," alisema Malugu.

Aliishukuru Plan International kwa ufadhiri huo, kwani hapo kabla vikwazo dhidi ya kinamama vilikuwa vingi, vikiwamo baadhi kujifungulia nyumbani au barabarani kutokana na kuchelewa kufika katika vituo kwa wakati kwa sababu ya umbali mrefu.

Mkurugenzi wa Miradi wa Plan International, Peter Mwakabale, alisema mradi huo ulianza kutekelezwa miaka 3 iliyopita na unatarajia kumalizika Juni mwaka huu.Stephano Kaliwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mlimba, alisema jitihada za halmashauri katika kutekeleza sera ya afya zinaendelea kuchukuliwa, ikiwamo kuendelea na ujenzi wa hospitali ya wilaya, na kwamba serikali kuu ilishatoa Sh. milioni 500 kukamilisha ujenzi huo ambao unatarajiwa kukamilika hivi karibuni na hospitali kuanza kutoa huduma mwezi ujao.



Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali, Charles Mbuge (wa pili kushoto), akifungua jengo la bwalo la askari katika Kikosi cha 844 JKT Itende, jijini Mbeya juzi. Kulia ni Kaimu Mkuu wa Utawala wa jeshi hilo, Kanali Hassan Mabena. PICHA: RENATHA MSUNGU

# Vitambulisho 59,000 kupewa wajasiriamali

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

UONGOZI wa Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mkoani humo umeweka utaratibu utakaowawezesha kusambaza vitambulisho 59,000 vya wajasiriamali wadogo walivyopata mwaka huu.

Taarifa hiyo imetolewa jana na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Peres Magiri, wakati akifungua kikao cha kupeana utaratibu wa usambazaji wa vitambulisho vya wajasiriamali vya mwaka 2021.Alisema lengo la kikao hicho ni kutaka zoezi hilo lifanyike kwa ufanisi na vimalizike mapema.

Pia alisema chini ya utaratibu wa mwaka huu, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, imepangiwa vitambulisho 7,670, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega (9,440), Nzega (9,440) na Uyui 9,440.

Alisema Manispaa ya Tabora imepangiwa vitambulisho 9,440, Sikonge (4,130), Urambo (4,720) na Kaliua (4,720).

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Tabora, Thomas Masese, alisema mfanyabiashara mdogo anatakiwa kuwasilisha maombi yake kupitia tovuti ya Ofisi ya Rais Tawala Mikoa na Serikali za Mitaa na kwa wale ambao watashindwa kujisajili kwa njia ya tovuti wafike Ofisi za Halmashauri zao kwa ajili ya msaada.Alisema mwombaji baada ya kukamilisha usajili atapatiwa namba ya malipo kwa ajili ya ada ya kitambulisho ambayo ni Sh. 20,000 malipo yanayotakiwa kufanywa kwa njia ya benki au simu za mkononi.

Masese alisema baada ya TRA kupokea maombi itachapisha vitambulisho na kuvipeleka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambaye naye atavipeleka kwa wakuu wa wilaya na kuvikabidhi kwa wakurugenzi watendaji.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara ambao mitaji yao ya mauzo kwa siku inazidi Sh. 10,500, kutochukua vitambulisho hivyo badala yake wafuate utaratibu wa kupata leseni za biashara.

Ofisa Biashara Mkoa wa Tabora, Alex Mhanga, alisema kwa mwaka 2018/19 walipata vitambulisho 65,000 na kuwezesha kupatikana Sh. bilioni 1.3, mwaka 2020, mkoa ulipata vitambulisho 71,500 na walifanikiwa kusambaza vitambulisho 60,390 na Sh. bilioni 1.2 zilipatikana.

# Bil. 200/- kutumika Simiyu 2021/2022

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKOA wa Simiyu umetenga Sh. bilioni 200 katika mwaka wa fedha 2021/2022, ambazo zinatarajia kutumika katika shughuli za maendeleo, matumizi ya kawaida pamoja na mishahara kwa watumishi ndani ya sekretarieti ya mkoa.

Hayo yalisemwa jana mjini Bariadi na Katibu Tawala Msaidizi ( mipango na uratibu), katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Donatus Weginah, wakati akitoa taarifa kwenye Kikao cha Ushauri cha Mkoa (RCC).

Weginah alisema makisio ya mamlaka za serikali za mtaa ni Sh. bilioni 13.7 zikiwamo Sh. bilioni 66.6 za miradi ya maendeleo, Sh. bilioni 111.3 kwa ajili ya mishahara na Sh. bilioni 13.7 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji safi Vijijini (RUWASA), Renatus Guma, alisema kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wanatarajia kutumia Sh. bilioni 18.4 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 1.9 sawa na asilimia 11.8 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alizitaka halmashauri zote kuendelea kubuni vyanzo vya mapato, huku akitolea mfano Halmashauri ya Maswa, ambayo alisema imekuwa mstari wa mbele kwa mambo mengi, vikiwamo viwanda.

# Neema yanukia 1,000 kupata maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI takribani ya 1,000 wa maeneo ya Kinyerezi, Mongo la Ndege, Kifuru na Vindini wanatarajiwa kuondokana na adha ya upatikanaji wa maji, baada ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kukamilisha kazi ya kuunganisha bomba kubwa la inchi 10 maeneo ya daraja la Kinyerezi.

Akizungumzia kukamilika kwa kazi hiyo jana, Meneja wa Usambazaji, Mhandisi Tyson Mkindi, alisema bomba hilo litakalopokea maji kutoka kwenye mradi mkubwa wa maji wa Pugu-Gongo la Mboto, na kwamba kazi iliyofanyika ni kubadilisha mtandao wa maji uliokuwepo kwa kuweka bomba jipya.

"Kazi iliyofayika ni kuweka bomba la inchi 10 litakaloweza kupokea na kusambaza maji kwa ajili ya kuhudumia wakazi wa maeneo ya Kinyerezi, Mongo la Ndege, Kifuru na Vindini, kazi hiyo imekamilika na baada ya kukamilisha kujenga mtandao tutaruhusu maji yaweze kufika kwa wananchi," alisema Mkindi.


Mama Samia alivyoanza siku tano Tanga Ukurasa 12





Ukurasa 13

**Sakaya: Uchaguzi mkuu uliopita umenipa ari ya kujipanga zaidi**



Ukurasa 14

**Kanali Besigye: Swahiba wa Museveni tangu porini, leo wako 'paka na panya'**



CHIFU NKOSI MHARULE

# Kaburi lake limebeba maajabu, duniani kote wamiminika kuhiji

• Atoka Afrika Kusini, azikwa na wawili hai

**Na Gideon Mwakanosya,**

SONGEA

MOJA ya vivutio vya utalii wa utamaduni vinavyopatikana katika Kijiji cha Mbingamharule wilayani Songea Mkoa wa Ruvuma, ni kuwapo kaburi la duara, ambalo Chifu Nkosi Mharule Bin Zulu Gama alizikwa mwaka 1889.

Ni mambo ambayo yanawashangaza wengi wanaotembelea kaburi hilo, hasa kwa historia inayoonesha kuwa Nkosi Mharule baada ya kufariki, alizikwa kwa desturi na mila za kichifu za kabila la wangoni toka Afrika ya Kusini, ndani yake kukiwapo mengi ya kutisha.

Christian Ngonyani, mwenye umri wa miaka 87 ni mzee wa mila kutoka Kijiji cha Mbingamharule, anayesema kijiji hicho kimepewa jina la chifu huyo, ambaye alitoka nchini Afrika Kusini na kutawala kuanzia mwaka 1847 hadi 1889, alipofariki na kuzikwa kijijini hapo.

"Chifu Mharule baada ya kufa mwaka 1889, alizikwa kwa taratibu za jadi ya machifu wa Afrika ya Kusini. Kaburi lake lilikuwa mviringo, sanda yake ilikuwa ya ngozi, alikalishwa kwenye kiti cha ngozi. Walikamatwa watu wawili wakiwa hai walizikwa naye wakiwa wamesimama mbele na nyuma ya Chifu," anasimulia Mzee Ngonyani.

Anazitaja taratibu za kijadi za wakati huo, zilitaka Mfalme au Chifu anapofariki, ni lazima azikwe na watu wawili, wakiwa hai na anasisitiza kuwa hiyo ilikuwa amri ya serikali ya jadi na hapakuwepo wa kulipinga.

Kwa mujibu wa Mzee Ngonyani, wengi waliokuwa wanazikwa wakiwa hai na mfalme, ni wale ambao walikuwa wamezoeana na kufanya kazi naye kwa karibu.



Kaburi la Chifu Nkosi Mharule Bin Zulu Gama. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

Hata hivyo, anaesema kaburi hilo linatumiwa na wananchi wa kijiji hicho kwenda kuhiji kila mwaka, kwenye kaburi ambalo lipo umbali wa kilomita mbili toka kijijini hapo.

Kwa mujibu wa Mzee Ngonyani, ndugu wa Chifu Mharule toka nchini Afrika ya Kusini, huwa wanafika mahali hapo kufanya matambiko kwenye kaburi hilo la ndugu yao.

Anasema, mwaka juzi ukoo wa Mharule kutoka Afrika Kusini walifika kushuhudia kusimikwa kwa Chifu Nkosi Imanuel Zulu Gama wa Tano, ambaye ndiyo chifu wa wangoni wa sasa.

Ngonyani anasema yeyote ambaye anapenda kwenda kutembelea kaburi hilo, kuna taratibu zake maalum za kimila, anazozitaja kuwa ni kubeba unga wa muhogo, mahindi na ulezi, uliotengenezwa na bibi katika kijiji hicho.

Baada ya kufika eneo la kaburi, huwa anatangulia mhusika ambaye anawasiliana na chifu kwa lugha ya jadi ndipo wanaitwa waliofika kutambika na kupiga magoti juu ya kaburi na kuomboleza kwa sala za jadi.

Hapo Ngonyani ana simulizi zake: "Baada ya maombi, kuku au mbuzi wanachinjwa juu ya kaburi la Chifu Mharule, jambo la kushangaza mbuzi anapochinjwa hapigi kelele, baada ya kuchinja mmoja anamwaga unga wote juu ya kaburi."

Hata hivyo, anasema ukifika asubuhi juu ya kaburi hauoni damu wala unga, vyote vinakuwa vimeliwa na kwamba hiyo ndiyo ishara ya kukubaliwa shida zote ambazo ulikwenda kuomba kwenye kaburi hilo.

Agnes Ngonyani, kiongozi wa kimila Msaidizi wa Mzee Ngonyani, anasema wamekuwa wakipokea wageni wengi wanaotembelea kaburi la Chifu Mharule kutoka nchi za Ulaya, Marekani na Afrika, ambako wanakwenda kwa shida mbalimbali, zikiwamo kuhiji na kufanya matambiko.

"Nimekuwa nikiwapeleka watu wa kawaida, waganga wa jadi, watalii na wagonjwa wanaenda kufanya maombi kwenye kaburi la Chifu na kufanikiwa," anasimulia Mama Ngonyani.

SIASA

# Mama Samia alivyoanza siku 5 Tanga

## • Ajadili dai la RC, Kabuku kuwa mji mdogo • Timu mawaziri waeleza 'tunaendaje' • Jengo jipya Handeni laokoa bil.2.6/-



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akizungumza na wananchi wa Mkata, aliposimama kuwasalimia juzi Jumatatu, katika siku ya kwanza ya ziara yake mkoani Tanga. **PICHA: MASHAKA MGETA**

**Na Mashaka Mgeta**, HANDENI

JUZI Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameingia mkoani Tanga, kuanza ziara ya siku tano yenye takribani saa 120.

Samia, anathibitisha kwamba licha ya kutofanya ziara kikazi, lakini alifika mkoani Tanga mara kadhaa kwa majukumu mengine katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi kilichopita.

Juzi Makamu huyo wa Rais alipokewa katika eneo la Mkata. Alianza kwa kukagua ujenzi wa jengo la ghorofa mbili la Halmashauri ya Wilaya ya Handeni lenye vyumba 209 na kumbi mbili zenye uwezo wa kuingiza watu 280 kwa mara moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, William Makufwe, anamjulisha Makamu wa Rais Samia, kuwa ujenzi ulianza mwaka 2019 kwa kufanyiwa usanifu wa awali ulioonyesha gharama hadi kukamilika zingekuwa Sh. bilioni 7.9, lakini kutokana na matumizi ya mfumo uitwao 'force account' ambao mifumo ya kiserikali hutumika kuokoa bajeti; gharama hizo zilishuka kufikia Sh. bilioni 5.3, hivyo kuokoa Sh. bilioni 2.6.

Ni mfumo unaotumika kwa mteja (halmashauri) kununua vifaa vya ujenzi moja kwa moja kwa mzalishaji au msambazaji, kwa kuzingatia na kujali thamani ya fedha dhidi ya shughuli husika.

Samia anasema Tanzania ina uongozi madhubuti unaojali maendeleo na ustawi wa jamii, hivyo anawahimiza wananchi 'kuchapa kazi'.

"Mjiepushe sana na malumbano, majibizano yasiyo ya msingi na mambo ya kwenye mitandao, Watanzania inatupasa kushikamana, tusivurugwe na mambo mapya yanayoingizwa nchini mwetu," anasema.

> Mjiepushe sana na malumbano, majibizano yasiyo ya msingi na mambo ya kwenye mitandao, Watanzania inatupasa kushikamana, tusivurugwe na mambo mapya yanayoingizwa nchini mwetu.

Makamu wa Rais anaendelea:"Zipo changamoto zinazoshughulikiwa kwa ufanisi mkubwa na watendaji wa serikali katika ngazi za msingi, wilaya, mkoa na Taifa, jambo la msingi hapa ni kwa Watanzania kuzidi kuungana, kushirikiana na kuchapa kazi."

Anaongeza: "Sisi (Tanzania) hatutengenezi fedha, bali tunazalisha kupitia kodi na ushuru vinavyotokana na ubunifu wetu na kuchapa kazi kwa bidii."

Anasema viongozi wa kiserikali wamekuwa mfano bora katika kutimiza wajibu, bidii kazini, kutatua kero za wananchi na kuhakikisha kunakuwapo matumizi sahihi ya rasilimali, hivyo kuchochea kasi ya maendeleo na ukuaji uchumi.

Samia anawaambia wananchi kwamba, matokeo ya utafiti wa kiuchumi kimataifa, unaielezea Tanzania kushika nafasi ya 10 katika nchi zinazoonyesha kasi kubwa ya ukuaji uchumi duniani.

Anayataja kuwa mafanikio yenye nafasi kukua zaidi, hata kuiwezesha nchi ikapanda nafasi za juu zaidi, iwapo wataendelea kushikamana na kufanya kazi kwa bidii.

### 'JAMBO LAO' KABUKU

Mtu anapopataja Kabuku, ni eneo maarufu barabarani penye biashara nyingi, kituo cha magari na njia panda kuelekea kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mgambo, pamechangamka saa 24.

Hapo pia ni kata wilayani Handeni na ambako Makamu wa Rais, anajulishwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella, kuhusu wananchi wake wana 'jambo lao' linalohusu uhitaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo.

Mkuu wa Mkoa alilipasua hilo, akidokeza ni kati ya matokeo ya mzozo uliowahi kuibuka zaidi ya miaka mitano iliyopita, kuhusu mahali panapofaa kuwa makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya Handeni.

Hata hivyo, uamuzi wa mwisho uliofikiwa, ulielekezwa makao makuu hayo katika kata ya Mkata, umbali wa takribani kilomita 41 kutoka Kabuku.

Baada ya matokeo hayo yaliyoungwa mkono na wananchi wa Kabuku, ndipo lilipozaliwa hitaji la kuwapo Mamlaka ya Mji Mdogo.

Ni hali iliyomfanya Rais Magufuli, alipopita katika kata hiyo wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2020, aliwajulisha wakazi hao wa Kabuku kwamba analitambua 'jambo lao' na lingeshughulikiwa kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni zilizopo.

Wazo hilo, ndilo analolitamka Mama Samia akiwahutubia wakazi wa Kabuku na kusema, mchakato wa kufikia Mamlaka ya Mji Mdogo unapaswa kufanywa katika ngazi zote, kwa kufuata taratibu ili kupata suluhu yenye tija.

Anasema, iwapo Kabuku itaonekana kuwa na sifa na vigezo vinavyotakiwa, itafanywa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo, lakini ikibainika kuwapo upungufu unaokwamisha kufikia viwango husika, utatolewa ushauri wa hatua za kufikia ili kupewa hadhi hiyo.

### MAWAZIRI WANGURUMA

Katika ziara hiyo, Makamu wa Rais aliambatana na mawaziri kadhaa wa serikali, wakiwamo Ummy Mwalimu (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Muungano na Mazingira), Jumaa Aweso (Maji) na Naibu Mawaziri Mwanaidi Ali Khamis (Fedha na Mipango) na Exaud Kigahe (Viwanda na Biashara).

Kwa upande wake, Waziri Ummy anatoa rai kwa halmashauri za wilaya nchini, kutenga maeneo ya uwekezaji viwanda, ili kudhibiti athari za uharibifu wa mazingira na migogoro kati ya wawekezaji na wakazi wa maeneo husika.

Ni kauli ya Ummy, ambaye pia ni mbunge mkoani Tanga, baada ya Mama Samia kuzindua shughuli za uzalishaji kiwanda cha kuchakata mahindi, chakula cha mifugo na kusindika matunda cha Segera, wilayani Handeni.

Waziri Aweso, anazungumza katika eneo la Mkata kuwa serikali inaendelea kutekeleza azma ya kutatua kero za maji kwa ufanisi na anatoa mfano wa kata hiyo kuwa miongoni mwa zilizopiga hatua za utatuzi wa kero hiyo.

"Zamani Mheshimiwa Makamu wa Rais, viongozi wa serikali walipokelewa kwenye eneo hili (Mkata) na wananchi wenye madumu, kama ishara ya kero ya maji, lakini sasa kero imepungua kwa kiasi kikubwa na hapa hakuna dumu hata moja...tunaendelea kukabiliana na changamoto hii mpaka kufikia azma ya jumla ya kumshusha ndoo mwanamke," anasema.

Naibu Waziri Kigahe, anasema serikali inatekeleza vema sera za uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo vya kodi na visivyokuwa vya kodi, ili kuweka mazingira bora yenye kuwanufaisha wafanyabiashara, wananchi na serikali.

### FURSA KWA WAKAZI

Makamu wa Rais Samia, anasema shughuli za uwekezaji zinapaswa kugusa maisha ya kila siku ya wananchi, hasa wanaozunguka maeneo yenye uwekezaji.

Kutokana na hali hiyo, Makamu wa Rais Samia, anatoa wito kwa kiwanda cha kuchakata mahindi, chakula cha mifugo na kusindika matunda cha Segera, kutoa kipaumbele cha ajira zinazokadiriwa kuwa 600, kwa wakazi wa eneo hilo.

Anasema hatua hiyo ina maana ya kurejesha faida kwa jamii na itasaidia kuwafanya wakazi hao kukilinda kiwanda na mali zake, hivyo kuendeleza amani na utulivu ambazo ni miongoni mwa nyenzo muhimu kwa uwekezaji.

Katika ziara ya mkoani Tanga, Makamu wa Rais Samia anatarajiwa kutembelea pia wilaya za Korogwe, Muheza, Tanga, Pangani na Mkinga.

Anatarajiwa kukagua na kuzindua miradi ya maendeleo na Mwongozo wa Uwekezaji Mkoa wa Tanga.

***Mwandishi wa makala haya ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Handeni. Anapatikana kwenye simu namba +255 754691540***

MAKALA

# Sakaya: Uchaguzi mkuu uliopita umenipa ari ya kujipanga zaidi

**Na Sabato Kasika**

## • Aota kurejesha jimbo 'lake' kwa staili hii




Magdalena Sakaya. **PICHA: MAKTABA**

MNAMO Oktoba 28, mwaka jana, ulifanyika uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani na kushuhudiwa wagombea wa vilivyokuwa vyama vya upinzani wakianguka vibaya, chama tawala CCM kikiendeleza ushindi, safari hii ukiwa wa kishindo.

Katika uchaguzi huo, vyama vya upinzani CUF na CHADEMA, vilibahatika kupata ubunge katika majimbo mawili tu ya Mtwara Vijijini na Nkasi Kaskazini mkoani Rukwa.

CUF ilipata ushindi katika jimbo la Mtwara Vijijini, dhidi ya mwakilishi wake wa zamani aliyejitosa kutetea nafasi yake, na mwanamama Hawa Ghasia, huku CHADEMA, ikitwaa jimbo ambalo kwa muda mrefu liliongozwa na mwanasiasa machachari kutoka CCM, Ally Kessy.

Wabunge wote walioshindwa walikuwa wawakilishi wa muda mrefu bungeni, kabla ya kunasa katika uchaguzi uliopita, walipojitosa kutetea nafasi zao.

Katika tafsiri pana, ni uchaguzi ambao haukumwacha salama aliyekuwa mbunge wa Kaliua mkoani Tabora, Magdalena Sakaya. Alijikuta naye ameshindwa kutetea jimbo ambalo aliliwakilisha bungeni kwa miaka mitano.

Mama Sakaya, ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha CUF, alichaguliwa kuwa mbunge katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Katika mazungumzo yake na gazeti Nipashe wiki hii ilipotaka ufafanuzi wa mustakabali wa maisha yake na siasa, mwanasiasa huyo ana ufafanuzi wa kina kuhusu msimamo wake kwenye siasa na utashi wa jimbo anakotokea, hata kuliwakilisha katika msimu wa uchaguzi uliopita.

Yafuatayo ni mazungumzo ya 'ana kwa ana' na mwandishi wa makala hii. Fuatilia:

**SWALI: Baada ya kushindwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana, umevunjika moyo kuwania tena ubunge katika uchaguzi ujao wa mwaka 2025?**

**JIBU: Kwanza kabisa, kukata tamaa** ni adui wa maendeleo. Hivyo, mimi sijakata tamaa, badala yake bado nina ari ya kuwatumikia wana Kaliua na ninaendelea kufanya majukumu yangu ya siasa na kujipanga kwa ajili ya uchaguzi ujao, ili panapo majaliwa ya uhai, basi nijitose tena, kwa sababu wananchi wa Kaliua bado wananihitaji niwe mbunge wao.

**SWALI: Kwa kasi hii ya maendeleo inayofanywa na serikali, unadhani kwamba miaka mitano ijayo wananchi wa Kaliua watakuwa bado wanakumbuka kwamba kuna Sakaya wakuchague tena?**

**JIBU:** Nikuhakikishie tu kwamba, wananchi wa Kaliua wako nami na waanendelea kuwa nami tangu kumalizika kwa uchaguzi na ninaendelea kuwa nao karibu, kwani nao waliumia baada ya kuona uchaguzi wa aina hiyo, ambao ulisababisha wapate mbunge ambaye hawakutarajia.

Kwa jinsi walivyo karibu nami, wamenifanya niwe na ari ya kuendelea kujipanga kwa ajili ya baadaye. Binafsi sikati tamaa, siasa ni kama dini, kwa kuwa mtu huwezi kuacha dini eti kwa sababu mchungaji amehubiri vibaya. Hivyo, hata mimi siwezi kukata tamaa kutokana na kile kilichotokea katika uchaguzi uliopita.

**SWALI: Unadhani ni kipi ambacho umewafanyia wananchi wa Kaliua na kuwafanya waendelee kukukumbuka na kutamani kukurudisha uwe mbunge wao?**

**JIBU:** Sikuwa na diwani kutoka chama changu, lakini shughuli za maendeleo zilikuwa zinafanyika kama kawaida. Kwanza, niliwaunganisha wana Kaliua ili wawe wamoja kwa ajili ya kujiletea maendeleo na nikafanikiwa.

**SWALI: Ni maendeleo gani hayo ambayo ulichangia kuyaleta Kaliua wakati ukiwa mbunge?**

**JIBU:** Yapo mengi tu kuanzia kwenye elimu, afya kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Jimbo, ikiwamo kusaidia kuondoa tatizo la kutojua kusoma na kuandika, kujenga zahanati na vituo vya afya na mengine mengi kwa ajili ya wana Kaliua.

Hivyo, ninaamini kwamba bado wananihitaji. Kwa taarifa yako ni kwamba, hata Rais Dk. John Magufuli amewahi kunimwagia sifa kuwa ninachapa kazi vizuri na kuwataka wabunge wa CCM kunipa ushirikiano ninapofanya shughuli za maendeleo.

**SWALI: Kwa hiyo unachofanya kwa sasa ni nini ili kukuwekea mazingira ya ushindi katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka 2025?**

**JIBU:** Pamoja na kwamba mimi ni Naibu Katibu Mkuu wa CUF Taifa, bado ninaendelea kuwa karibu na wananchi wa Kaliua kwa kuwatembelea kila mara kusikiliza kero zao.

Kwa kweli wananitia moyo kwamba nisikate tamaa kwa yale yaliyotokea uchaguzi uliopita, bali niendelee kujipanga kwa ajili ya 2025. Nami sitawaangusha na kama panapo uhai na akawa hajatokea mtu mwingine wa CUF wa kutaka Jimbo la Kaliua, nitawania tena.

**SWALI: Iwapo atatokea mgombea mwingine wa CUF akawa anataka kuwania jimbo hilo utakuwa tayari kumpisha?**

**JIBU:** Jimbo si mali yangu, bali wakitokea watia nia wengine ndani ya CUF, watapitia kwenye mchujo wa vikao halali vya chama na hatimaye atateuliwa wa kuwakilisha chama chetu, kama nitakuwa mimi au mwingine, yote ni sawa, kwa sababu lengo ni kutaka Kaliua iwe chini ya CUF kama ilivyokuwa miaka mitano iliyopita.

> Pamoja na kwamba mimi ni Naibu Katibu Mkuu wa CUF Taifa, bado ninaendelea kuwa karibu na wananchi wa Kaliua kwa kuwatembelea kila mara kusikiliza kero zao.

**SWALI: Chama chako kimeshaweka wazi kuwa hakitashiriki uchaguzi wowote hadi kuwe na katiba mpya na tume huru ya uchaguzi. Sasa wewe kwanini unajipanga wakati chama hakina mpango wa kushiriki uchaguzi?**

**JIBU:** Suala la kujipanga ni muhimu, kwani ndani ya miaka hii iliyopo kabla ya uchaguzi mkuu, lolote linaweza kutokea, ikiwa ni pamoja na kuwapo katiba mpya na tume huru. Hivyo tuliache hilo kama lilivyo.

**SWALI: Una lipi la kuwaambia wanasiasa wenzako wa vyama vya upinzani?**

**JIBU:** Wasikate tamaa kwa yale yaliyotokea katika uchaguzi mkuu, watambue kuwa siasa ni mchezo mchafu, wajipange upya wakitambua kuwa mwisho wa uchaguzi, ndiyo mwanzo wa maandalizi ya uchaguzi mwingine.

Miaka mitano si mingi panapo uhai, hivyo suala la kujipanga mapema ni la muhimu. Siyo wakati wa kuendelea kulalamikia mambo ambayo tayari yamepita.

JUKWAA LA UONGOZI

# Kanali Besigye: Swahiba wa Museveni tangu porini, leo wako 'paka na panya'

• Rafiki, daktari na waziri wake • Kila mara jela • Chaguzi nne kashindwa kumng'oa, hatimaye ampisha Bobi Wine

**Na Christina Mwakangale**

Dk. Warren Kizza Besigye Kifefe; ni jina kubwa katika siasa za Uganda, hata wimbi la Afrika, mzaliwa wa Aprili 22 mwaka 1956, akiwa na fani kuu za udaktari wa binadamu, wasifu aliyoupata kwa miaka mitano ndani ya chuo kikuu.

Pia, huyo ni ofisa mwandamizi mstaafu wa jeshi kufikia ngazi ya kanali, stadi aliyopata katika vita vya porini na kisha mafunzo rasmi kijeshi na mwanasiasa.

Jingine la upekee kwake, ni rafiki wa Rais Yoweri Museveni, hata aliwahi kupewa wadhifa wa tabibu wake katika vita vya porini, kabla siasa hazijawatenganisha kuwa 'paka na panya' baada ya miaka 17 ya kuwa pamoja kiswahiba.



Dk. Kizza Besigye. **PICHA: MTANDAO**

**ALIKOTOKEA**

Ana historia inayoanzia katika Manispaa ya Rukungiri, Kusini Magharibi mwa Uganda, alikozaliwa mtoto wa pili kati ya sita kifamilia.

Bahati mbaya baba yake aliyekuwa polisi na mama yake, wote walifariki hata kabla hajamaliza madarasa ya awali.

Aliendelea na Shule ya Msingi Mbarara Junior, kabla ya kuendelea na sekondari jijini Kampala, alikomaliza kidato cha nne na kisha kidato cha tano na sita, wilayani Kabale.

Mwaka 1975, Uganda ikiwa chini ya Rais Iddi Amin, alijiunga na Chuo Kikuu cha Makerere kwa masomo ya udaktari wa binadamu na alihitimu mwaka 1980, Iddi Amin tayari alishang'olewa.

Baada kuhitimu, alitumikia kwa muda mfupi katika Hospitali Kuu ya Mulago jijini Kampala (kama Muhimbili), pia akiwa na nyendo za kisiasa kwa siri, hata akalazimika kukimbilia uhamishoni nchini Kenya ndani ya muda mfupi.

Huko ndiko alikoomba usajili rasmi wa udaktari na aliajiriwa katika Hospiali ya Aga Khan jijini Nairobi na kisha alihamia Hospitali Kuu ya Kenyatta (kama Muhimbili).

Hata hivyo, nafasi yake ilijaa utashi wa siasa kwa siri na mwaka 1982, aliamua kujiunga na vikosi vya NRM chini ya Museveni, katika vita vya porini, jukumu mojawapo alilopewa ni daktari binafsi wa Kamanda Mkuu, Museveni.

Nyendo za Museveni kwa jina la National Resistance Movement and Army (NRM/A), zilipochukua madaraka mnamo Januari 1986, Dk. Besigye, wakati huo alikuwa kijana wa miaka 29, aliteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia siasa.

Nyendo za kijeshi za NRM ndizo baadaye zikabeba wasifu wa kuwa chama cha kisiasa, kinachoendelea hadi sasa.

> Kuna wakati alikuja na hoja dhidi ya sheria kali iliyopitishwa dhidi ya ushoga Uganda, yeye akiwania haja ya kuunga mkono kuwa wana haki.

Mwaka 1991, Dk. Besigye alirejeshwa katika madaraka ya kijeshi, kuwa mdhibiti kikosi cha Masaka katikati ya Uganda na miaka miwili baadaye, akapatiwa madaraka zaidi ya kusimamia maghala na uhandisi.

Wakati akiwa mwanasiasa mwandamizi nchini Uganda, Julai 1999, Dk. Besigye akiwa na miaka 43, alifunga ndoa na Winnie Byanyima, Mbunge wa Jimbo la Nsambya na mwanasiasa machachari, wakapata watoto wawili.

**SIASA PINZANI**

1999 ndio mwaka uliomtenganisha rasmi Kanali Dk. Besigye na swahiba wake, afande na Rais wake, Yoweri Museveni, alipochapisha waraka ulioiponda uongozi wa NRM, ikiashiria wakianza kutofautiana kwa siri.

Alichukuliwa hatua katika Mahakama ya Kijeshi akiamrishwa kuomba msamaha kwa kuchapisha nyaraka ya namna hiyo kwa umma, akasamehewa.

Ikiwa hana muda mrefu tangu apandishwe cheo cha kanali, alitangaza kustaafu jeshini, huku akitangaza azma ya kujitosa katika uchaguzi mkuu wa nchini Uganda mwaka 2001, dhidi ya Rais Museveni.

Besigye alianza vuguvugu la kampeni, akiupinga uongozi wa nchi kwa madai kujaa rushwa na urasimu, akiahdi kuingia madarakani kama chombo cha kujenga kipindi cha mpito cha kuunda usahihi wa siasa ya vyama vingi.

Alishindwa katika uchaguzi huo ambao aliunda umoja na vyama vingine vya nchini Uganda mwaka huo 2001 na waliambulia asilimia 28 tu ya kura zote.

Baadaye, Dk. Besigye aliendа mahakamani kupinga matokeo, lakini uamuzi wa majaji watatu hawakukubali ombi lake kubatilisha matokeo.

Miezi mitatu baada ya matokeo, Juni 2001 alianza kukumbwa na misukosuko alipotuhumiwa na serikali kuhusiana na magaidi wa PRA walioko porini wakati huo upande wa Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC).

Baada ya miezi miwili alitoroka nchi na kwenda uhamishoni Afrika Kusini kwa miaka minne, akidai kuhofu usalama wake. Hata hivyo, hakukaa kimya, aliendelea kuuponda uongozi wa Uganda.

Ulipotimu msimu wa kampeni za uchaguzi Oktoba 2005, akidhamiria kujisajili kwa uchaguzi wa mwaka 2005, alirudi na kulakiwa na mamia ya wafuasi wake katika uwanja wa ndege, jambo lililoashiria bado kuwa na umaarufu kisiasa nchini Uganda.

Kurejea kwake, hata baada ya kujisajili kwa kampeni zake hakukumuacha salama.

Alikumbwa na matukio tofauti ya kukamatwa mara 14, akinyooshewa vidole vya kuhusika na jinai, kuwekwa ndani hata kushitakiwa wakimhusisha na waasi wa Lord's Resistance Army (LRA).

Hata hivyo, jumuiya za kimataifa zilikuja juu mara kadhaa kuingilia kati suala hilo, hata kuwezesha kampeni kuendelea, huku kukiwapo wafuasi waliokuja juu kuhusu kukamatwa kwake, hata mamlaka za dola kushindana nao, pale walipoleta rabsha.

Akiwa katika muungano na vyama vingine kama vile Uganda People's Congress (UPC) na Democratic Party (DP), Dk. Besigye alipata asilimia 37 ya kura dhidi ya asilimia 59 za Museveni. Pia, alienda mahakamani kupinga matokeo, lakini hakufanikiwa.

Mwaka 2011 aliingia tena katika uchaguzi, ushawishi wake ukionekana kushuka zaidi na akashindwa dhidi ya Rais Museveni na uchaguzi wa mwaka 2016, hali ilifanana na hiyo.

Baada ya matokeo hayo ya 2011, aliwaamuru wabunge wake waliochaguliwa kususia kikao cha bunge, ingawa hawakukubaliana naye.

Mara nyingine aliandaa maandamano kupinga kupanda bei ya vyakula, hata akakutana na misukosuko mikali dhidi ya vyombo vya dola, baadhi kuwekwa ndani na kuwapo vifo.

Kuna wakati alikuja na hoja dhidi ya sheria kali iliyopitishwa dhidi ya ushoga Uganda, yeye akiwania haja ya kuunga mkono kuwa wana haki.

Katika uchaguzi mkuu uliopita Dk. Besigye, alitangaza hatowania tena wadhifa huo na wafuasi wa chama chake cha FDC kwamba, baada ya kutafakari kwa kina ameona kutoa nafasi kwa mtu mwingine.

Wachambuzi wa siasa, wanasema ni uamuzi uliotoa nafasi kwa kijana Robert Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, aliyeonekana kuungwa mkono zaidi na vijana wengi, hasa waishio mijini.

Ni sehemu ya kundi lililomuunga mkono zaidi katika uchaguzi haswa wa mwaka 2001, pia 2005.

Mwaka 2019, Bobi Wine na Dk. Besigye waliahidi kushirikiana kuondosha madarakani chama tawala, NRM kinachoongozwa na rais Yoweri Museveni. Hata hivyo, alishindwa

***Makala hii imeandaliwa kwa msaada wa taarifa mbalimbali.***





# Katambi afanya uamuzi mgumu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, amemuagiza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), William Erio kuwasimamisha kazi watumishi wawili kwa kushindwa kuidai michango ya wafanyakazi wa kampuni ya Kiribo ya mkoani Mara, hadi kufikia deni la Sh. bilioni 1.1.

Pia, ameagiza kusimamishwa kazi Ofisa Kazi wa Mkoa wa Tabora, Revokatus Mabula kwa tuhuma ya matumizi mabaya ya madaraka.

Katambi alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu ziara yake aliyoifanya mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Aliwataja watumishi hao ni wa NSSF mkoani Mara ambao ni Maneno Mpogole na Abdulabi Salehe, wanaodaiwa kushindwa kutimiza majukumu yao kudai madeni ya kampuni hiyo hadi kufikia Sh. bilioni 1.1, huku ikionyesha fedha hizo zilikuwa hazifuatiliwi.

"Pia kuna kampuni ndogo zinazofanyakazi na mgodi wa North Mara zimekuwa na udanganyifu mkubwa sana... kwa mfano, kampuni ya Kiribo kushindwa kulipa wafanyakazi zaidi ya Sh. milioni 300 na kukwepa kulipa kodi na fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii hadi kufikia Sh. bilioni 1.1 na kodi ya sh. bilioni moja ambazo zingelipwa kwa Serikali," alisema.

Aliagiza mamlaka za Mkoa wa Mara kuufikisha Dodoma uongozi wa mgodi huo na mmiliki wa Kampuni hiyo ili kulipa madai hayo na kulipa kodi ya Serikali.

Aliwaagiza mameneja wengine wa mikoa kufuatilia madeni wanayodai kwenye taasisi za binafsi na za Serikali kuhakikisha madeni yanakusanywa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Kadhalika, alisema katika mgodi huo wa North Mara amebaini udanganyifu mkubwa hasa kwa wageni kufanyakazi bila kuwa na vibali vya kazi, jambo ambalo ni kinyume cha taratibu za nchi.

"Pia nimekuta kazi wanazofanya zingeweza kufanywa na Watanzania na taarifa inaonyesha kazi hizo zinafanywa na wazawa, kulikuwa na udanganyifu mkubwa kwa kushirikiana na kamati ya ulinzi na usalama tuliweka mtego na kubaini raia wa kigeni wakifanyakazi ambazo zingefanywa na wazawa," alisema.

Alisema walinasa raia wa kigeni akifanya kazi za ununuzi na huduma za malipo na kubaini wengine tisa wakifanya kazi bila kuwa na vibali.

Aliagiza maombi yote ya vibali yaombwe kwa Kamishna wa Kazi ili kuepuka vishoka.

Kuhusu Ofisa Kazi wa Tabora, Katambi alifafanua kuwa Ofisa huyo wakati akiwa Mkoa wa Shinyanga kabla ya kuhamishiwa Tabora, anatuhumiwa kushindwa kusimamia majukumu yake vyema.

"Nimebaini mtumishi huyo alikuwa akiwahujumu wafanyakazi na kuwa upande wa waajiri, hivyo kushindwa kusimamia wafanyakazi na haki zao, na baada ya kubaini mambo hayo nikiwa kwenye uchunguzi niligundua jioni ya siku hiyo aliita waandishi wa habari wasitoe habari hiyo," alisema.

Aliagiza Mamlaka iliyomteua kumchukulia ili iwe mfano kwa wengine.

Pamoja na hayo, Katambi katika ziara yake alibaini mgodi wa Elhilal wa Shinyanga kuna baadhi ya wafanyakazi 35 wa mgodi huo wanadai kampuni hiyo Sh.milioni 80 za michango iliyopaswa kuwasilishwa NSSF.

Kaimu Kamishna wa kazi, Andrew Hebron, aliahidi kuyafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na Katambi.



Mratibu wa Mradi wa Elimu Jumuishi unaosimamiwa na Kanisa la Free Pentecostal Church Tanzania, Jane Mgidange, akiagana Bahati Erenest (15) ambaye ana ulemavu wa viungo wa Kijiji cha Bahi, mkoani Dodoma juzi, baada ya kumpatia msaada wa vitu mbalimbali zikiwamo nguo. Kutoka (kushoto) ni Diwani wa Kata ya Bahi, Augostino Leonard, wazazi wa mtoto, Elimia George na Paskali Kalungiro na mlezi wa mradi huo, Mch. Daud Msaghaa. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Maofisa ununuzi wakumbushwa sheria

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MAOFISA ununuzi nchini wametakiwa kutokiuka taratibu na sheria za manunuzi ili kuepusha upotevu wa fedha ili kukamilisha miradi kwa ufanisi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alitoa angalizo hilo juzi alipokuwa akifungua mafunzo ya sheria ya manunuzi ya umma kwa maofisa hao kutoka idara mbalimbali nchini yaliyofanyika, jijini hapa.

Alisema maofisa hao wanapaswa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya manunuzi ya umma inayotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) ili manunuzi yanayofanywa yawe na tija na kupata thamani halisi ya fedha.

"Matarajio yangu mimi naangalia matokeo, natarajia kuona kasi kubwa ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya serikali kwa sababu maeneo mengi unaweza kukuta shughuli za utekelezaji zimekwama kwa sababu ya manunuzi yamechukua muda mrefu," alisema.

Akizungumzia malengo ya mafunzo hayo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Leonard Kapongo, aliwataka watendaji hao kutumia mafunzo hayo kuongeza ufanisi kwenye maeneo yao ya kazi.

Pia, aliwasisitiza watu hao wanaoshughulikia masuala ya manunuzi kuwa waadilifu ili manunuzi wanayofanya yawe na tija. "Sisi tunaamini kwa kujengeana uwezo, wataelewa na weledi utaongezeka katika utendaji kazi wao," alisema.

## Katazo biashara maeneo yasio rasmi lasisitizwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

VIONGOZI wa masoko Jiji la Dodoma wametakiwa kuwaelimisha wafanyabiashara wenzao kuacha tabia ya kutangatanga na kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alitoa maelekezo hayo alipokuwa akizungumza na viongozi wa soko la Makole alipofanya ziara ya kuwatembelea na kuona shughuli za kibiashara.

Alisema badala ya kuwaacha wafanyabiashara hao wakitangatanga kwa kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi, viongozi hao wanatakiwa kuhamasisha kufanya biashara kwenye maeneo yaliyotengwa na Jiji ili kupata fursa ya mikopo itakayokuza mitaji yao.

Yuna alisema baadhi ya viongozi ndani ya masoko wamekuwa vinara wa kuwaongoza wafanyabiashara kutangatanga kwenye maeneo ambayo Halmashauri ya Jiji imeshatoa angalizo la kutofanya biashara.

"Ninawaomba nyinyi viongozi wa soko hili la Makole tumieni nafasi zenu kukaa pamoja na wafanyabiashara mjue namna gani ya kuziona fursa zitakazojitokeza kwenye soko lenu hili, badala ya kutangatanga kwenye maeneo mengine ambayo yameshapigwa marufuku kufanya biashara zenu," alisema.

Mwenyekiti wa soko hilo jipya la mboga na matunda la Makole, Hamida Maftaa, aliwataka viongozi wa masoko kuwa mabalozi kwa ajili kuwasaidia watendaji wa halmashauri hiyo.

Alisema bado kuna maeneo mengi si rafiki kwao hali ambayo inayowafanya wafanyabiashara wa soko hilo kuwa na tabia ya kutangatanga kwenye masoko mengine. Aliomba Halmashauri hiyo kuendelea kutoa elimu na ushirikiano ili kuboresha biashara na kuondokana na tatizo la wafanyabiashara kuvamia maeneo yasiyo rasmi.





# Watembea umbali mrefu kusaka maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa vijiji vinne vya Kata ya Tembela katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanalazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilomita moja kwenda kutafuta huduma ya maji kwenye mito na chemichemi kutokana na vijiji hivyo kutokuwa na maji ya bomba.

Wakizungumza na Nipashe juzi, wananchi hao walisema vijiji vyao havijawahi kupata huduma ya maji ya bomba na hivyo wanalazimika kunywa maji ambayo usalama wake ni mdogo kutokana na kuchangia na wanyama.

Baadhi ya wanawake wa vijiji hivyo, walisema tatizo hilo la maji limekuwa likihatarisha maisha yao kutokana na kuamka usiku na kutembea kwenye maeneo yenye misitu.

Mmoja wa wanawake hao, Gulila Kasege, mkazi wa Kijiji cha Simambwe, alisema kutoka nyumbani kwake mpaka maji yanakopatikana, ni zaidi ya kilomita tatu na kuna milima na vichaka ambavyo vinatishia usalama wake.

Alisema wakati mwingine huwa wanaviziwa na vibaka hasa kipindi hiki ambacho mahindi yamekuwa marefu, hali ambayo inawafanya wawe wanahamasishana kwenda kwa makundi ili kuepuka kudhurika.

"Huwezi kwenda peke yako. Kwa hiyo, huwa tunaitana angalau tuwe watano ndiyo tushuke kule bondeni kuchota maji, lakini pia sasa hivi ni msimu wa mvua kuna utelezi njiani unaweza ukateleza ukaumia na ukiwa mjamzito, mimba inaweza ikatoka huko huko," alisema.

Gulila aliiomba serikali iwasaidie kusogeza huduma hiyo kama ilivyofanya kwenye maeneo mengine nchini, ili dhana ya kumtua mama ndoo kichwani ionekane kila mahali.

Martha Mwinuka, mama lishe katika Kijiji cha Simambwe, alisema tatizo la ukosefu wa maji kwenye kijiji hicho linawafanya kutopata faida kwenye biashara hiyo kutokana na kulazimika kutumia pikipiki kufuata maji.

Alisema ili maji yawafikie kwenye eneo hilo, wanalazimika kukodi pikipiki kwa gharama ya kati ya Sh. 2,000 na 2,500 na kwamba wakitaka kufuata wenyewe, huwa wanatumia zaidi ya saa moja kurejea kazini kwao.

Alisema katika kijiji hicho wanalazimika kuvuka Barabara Kuu ya Mbeya-Tukuyu hali ambayo huwa ni hatari hasa kwa watoto wanaofuata maji.

"Wakati mwingine huwa tunachota kijiji jirani ambako nako tunalipa kila mwezi na unatakiwa unapoenda uonyeshe risiti ya malipo ya mwezi uliotangulia na hata kama unamtuma dereva bodaboda, lazima umpatie na hiyo risiti," alisema Martha.

Diwani wa Tembela, Juma Mwakalobo, maarufu Mwadangala, alisema kata hiyo ina vijiji sita ambavyo ni Shibolya, Gari-Jembe, Simambwe, Ilembo-Usafwa, Isoha-Njiapanda na Ngoha.

Alisema kati ya vijiji hivyo, ni viwili pekee ambavyo angalau vinapata maji ambavyo ni Gari-Jembe na Ngoha ambavyo hata hivyo maji hayo bado hayatoshelezi mahitaji ya wakazi wake.

Alisema tatizo hilo limekuwa likimsumbua kutokana na wananchi kumlalamikia mara kwa mara wakitaka awafuate maofisa wa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) ili wajibu kero hiyo ya muda mrefu.

Alisema maofisa wa RUWASA waliwahi kufika katika kata hiyo wakazunguka na kutoa kauli za matumaini kwa wananchi lakini mpaka sasa hakuna utekelezaji

"Ilitakiwa tuyachukue maji kutoka Mto Nyalwela lakini bahati mbaya maji yale hayatoshi maana huwa yanapungua sana kiangazi.

"Maofisa wa RUWASA walisema watatuletea maji kutoka Mto Mlowo ambayo yatakuwa yanavutwa kwa mota na ninakusudia kuwafuata tena maana malalamiko ya wananchi ni mengi," alihidi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Stephen Katemba (kulia), akizungumza na wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya kati wanaoishi katika halmashauri hiyo jana, kuhusu mambo mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kujiajiri kwa kuanzisha miradi badala ya kusubiri kuajiriwa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## DED awafunda wahitimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, amewashauri vijana waliohitimu vyuo mbalimbali nchini, kuunda vikundi vya ujasiriamali, ili wanufaike na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ikiwamo mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotolewa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Stephen Katemba alitoa rai hiyo juzi alipozungumza na vijana, akiwataka kufikiria namna ya kuanzisha miradi itakayowafanya wajiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema halmashauri hiyo imekuwa ikitoa mikopo kwenye vikundi vya wajasiriamali kama sehemu ya kuwainua kiuchumi na kupunguza tatizo la ajira nchini na hivyo wasomi hao ni sehemu ya wanaostahili kunufaika.

"Mikopo hii haina riba yoyote na inarejeshwa kidogo kidogo. Sasa, ninawashauri mtumie hii fursa kuunda vikundi ili tuwakopeshe fedha muanzishe miradi badala ya kusubiri kuajiriwa na serikali au kampuni," alisema.

Katemba alisema maarifa waliyoyapata kwenye vyuo walivyosomea, yanatakiwa yaonyeshe thamani yao kwa kuwasaidia kuwa wabunifu hasa katika kipindi hiki ambacho serikali inasisitiza uchumi wa viwanda.

Alisema vijana hao wanaweza wakaanzisha viwanda vya kuchakata mazao mbalimbali, yakiwamo ya kilimo na ufugaji ili kujiongezea kipato na kuzalisha ajira.

# Bunge laipa mbinu wilaya kudhibiti moto hifadhini

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imeiagiza serikali kuhakikisha inashirikiana na wadau kudhibiti matukio ya uchomaji moto katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Mlima Rungwe wilayani Rungwe mkoani Mbeya, ili kulinda ikolojia ya mlima huo.

Agizo hilo lilitolewa juzi wakati kamati hiyo ilipozuru kwenye hifadhi ya msitu huo ambao unasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS).

Katika taarifa wa wakala huo, ilionyesha kuwa hifadhi hiyo imekuwa ikikabiliwa na tatizo la moto mara kwa mara.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Aloyce Kwezi, alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, kuvitumia vyombo vya dola kudhibiti moto huo ili kuipunguzia serikali gharama za utunzaji wa misitu hasa kurejesha ikolojia inayokuwa imeharibiwa.

Alisema mbali na kutumia vyombo vya dola, serikali inatakiwa kuwashirikisha watendaji wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo kwa kuwa wanaishi na wananchi kwa karibu zaidi na ni rahisi kuwashawishi.

"Mkuu wa Wilaya, kwenye taarifa tuliyosomewa, inaonyesha kuwa hifadhi hii inakumbwa sana na matukio ya moto. Sasa tunakuomba ushirikiane na watendaji wa vijiji na kata kudhibiti moto huu. Tunataka ikolojia hii iendelee kuwapo," Kwezi aliagiza.

Aliwataka wananchi wote wanaozunguka hifadhi za misitu nchini, kushiriki kutunza mazingira kwa kuepuka kukata miti ovyo na kuchoma moto kwa kuwa uwapo wa misitu hiyo ni muhimu kwa maisha yao.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Chalya, alikiri hifadhi hiyo kukabiliwa na matukio ya moto mara kwa mara huku akidai kuwa moja kati ya matatizo yanayowakabili, ni ubovu wa miundombinu ya barabara zinazoingia kwenye hifadhi hiyo.

Alisema wakati wa kukabiliana na matukio ya moto, ubovu wa barabara huchangia kuchelewesha watu kufika kwenye maeneo husika na hivyo kusababisha maeneo makubwa zaidi kuathiriwa.

Aliiomba kamati hiyo kusaidia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuongezwa bajeti ili isaidie kwenye ujenzi wa barabara hizo zitakazosaidia kukabili matukio ya moto kwenye misitu ya hifadhi.

"Kama mlivyoona wakati tunapandisha huku, barabara zetu siyo nzuri sana, tunaomba ikiwezekana TARURA watengewe bajeti mahususi ya ukarabati wa barabara hizi. Wakati wa matukio ya moto wakati mwingine tunachelewa kufika kutokana na ubovu wa barabara hizi," alisema Chalya.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, aliwataka Watanzania kutunza mazingira ikiwamo misitu ili kukabiliana na matatizo mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema misitu inasaidia kutunza vyanzo vya maji ambavyo vinatumiwa na Watanzania, inachangia mvua kuendelea kunyesha na kusaidia kuwa na hali nzuri ya hewa inayovutia kilimo.

"Pia, tunategemea kwamba barabara zikiboreshwa kwenye msitu huu, itakuwa miongoni mwa maeneo ya kuhamasisha utalii wa ndani na wa nje," alisema.

Masanja aliwataka maofisa wa TFS kuendelea kuimarisha ujirani mwema na wananchi wanaoishi kuzunguka misitu ya hifadhi ili wawe sehemu ya wahifadhi.





Kamishna wa Kazi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Fatma Iddi Ali (aliyekaa katikati), akizungumza na wafanyakazi wanaojenga mabwawa ya umwagiliaji maji yalioko Kibokwa, Wilaya ya Kaskazini A" Unguja, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi asema haridhishwi na uendeshaji wa sekta ya utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema haridhiki na sekta ya utalii inavyoendeshwa hasa ikizingatiwa kwamba ndiyo tegemeo kwa uchumi wa Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu jijini Zanzibar juzi alipokutana na uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale na baadhi ya watendaji wa wizara katika mkutano maalum wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maagizo waliyopewa mawaziri pamoja na makatibu wakuu wakati wa hafla ya kuapishwa.

Alisema uchumi wa Zanzibar kwa kiasi kikubwa unategemea sekta ya utalii lakini bado hajaridhika unavyoendeshwa na kuna haja ya mambo mengi kufanywa kinyume na ilivyo hivi sasa.

Rais Mwinyi alisema miongoni mwa juhudi ambazo zinahitajika kwa kiasi kikubwa ni kuitangaza zaidi sekta ya utalii ili kuona maendeleo yanapatikana kama ilivyokusudiwa.

Alisema dhima ya mikutano hiyo anayoiendesha Ikulu ni kurekebisha utendaji, hivyo kuna kila sababu kwa wizara kubadilika ili kuhakikisha sekta ya utalii inafikia malengo yaliyokusudiwa katika kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

Pia Rais Mwinyi alisema kuna haja ya kuwa na chombo maalum cha utalii kikiwa na azma ya kuimarisha uchumi wa visiwa hivyo.

Kuhusu makumbusho, alieleza haja ya kuyafanyia utaratibu maalum za makumbusho ya Zanzibar ambazo utawezesha kufanya kazi badala ya kuwa kama yalivyo hivi sasa kwa kuwa ni moja ya vitu vinavyochangia mapato ya utalii.

Pia, alisema kuna umuhimu wa kukusanywa fedha kwa njia ya elektroniki hatua ambayo itaondosha kupotea au kuvuja kwa mapato katika sekta ya utalii.

Kwa upande wa nyumba za Mji Mkongwe, Dk. Mwinyi aliitaka wizara hiyo kutafuta wawekezaji wa kuwekeza kwa baadhi ya nyumba walizozitenga sambamba na kuimarisha miundombinu ya mji huo ili uwe Mji Mkongwe wa kitalii.

Rais Dk. Mwinyi pia alisema ni vyema historia ikahifadhiwa na kwa wale waliovamia maeneo ya kihistoria waondoshwe.

Naye Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, aliitaka wizara hiyo kuimarisha miundombinu ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Waziri wa Wizara ya Utali na Mambo ya Kale, Lela Muhammed Mussa, alisema dhamana ya wizara hiyo ni pamoja na kusimamia sekta kuu mbili ambazo ni utalii na mambo ya kale ambazo hujumuisha kamisheni moja, idara nne, mamlaka moja na Ofisi Kuu Pemba.

Waziri Lela alisema miongoni mwa vipaumbele vya wizara kwa miaka mitano ijayo ni pamoja na kuibua vivutio vipya na kuimarisha vile vilivyopo ili kufikia lengo la wageni 850,000 na kuongeza siku za ukaazi kutoka siku nne hadi tisa ifikapo mwaka 2025.

Pia alisema baadhi ya sheria ambazo zinahitaji kurekebishwa hasa ikizingatiwa kwamba wizara hiyo inasimamia sheria tatu ambazo zinahitaji kufanyiwa mapitio ili ziende sambamba na mipango ya ukuaji uchumi ya kitaifa.

# Mkaguzi ataka tanuri kuchoma bidhaa bandia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKAGUZI Mkuu wa Dawa wa Wakala wa Chakula Zanzibar (ZFY), Muhidini Ahmada Mwadini, ameiomba Serikali ya Zanzibar kuweka tanuri la kuchomea bidhaa tofauti zikiwamo dawa za binadamu ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Muhidini aliyasema hayo juzi Kikungwi Wilaya ya Kati Unguja, baada ya kuangamiza dawa bandia zilizokamatwa hivi karibu katika ghala la Unguja Famasi zilipohifadhiwa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Alisema kuwapo kwa chombo hicho, kutarahisisha ufanyaji wa kazi tofauti na hali ilivyo sasa.

Hivi sasa, alisema wamekuwa wakitumia njia ya kuziponda kwa kutumia tingatinga na badaye huchomwa moto jambo ambalo si salama kiafya na kimazingira.

Pia aliwataka wananchi wanapokwenda kununua dawa katika maduka ya dawa kuwa waangalifu kwa kuangalia tarehe ya kumaliza matumizi yake ili kuepusha madhara yasiyokuwa ya lazima.

"Ni vyema wananchi wanapokwenda kwenye maduka ya dawa kuwa waangalifu na kuangalia muda wa kumaliza matumizi ya dawa hizi ili taifa kubaki salama na endapo wakigundua watoe taarifa sehemu husika," alisema.

Alisema dawa zilizoangamizwa ni za kikohozi (kifua) na za viungo ambazo mtengenezaji alikuwa anajaribu kuzifananisha na dawa zilizokuwapo katika soko la Zanzibar na wananchi wamekuwa wakitumia.

Alitaja baadhi ya dawa za kifua kuwa ni Cadiphen, Phamacofi na Vifex ambazo zipo katika soko Zanzibar na dawa iliyokuwa feki ni Cadifan, pharmkof, Indocin 25, Ungu Mp-Clox na Ungucam ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu.

"Dawa hizi zimekuwa zinafanana sana huwezi kuzitambua mara moja lakini ukiwa mtaalamu unazitambua ila sio kwa hafla pia huwezi kugundua," alisema.

Naye Mkuu wa Divisheni ya Ufuatiliaji na Operesheni ya Kimazingira, Subira Thabit, alisema katika kuangamiza dawa hizo, walilazimika kufuata miongozo na taratibu za kiuteketezaji.

Alisema walikwenda kuteketeza dawa hizo umbali na makazi ya jamii ili kuikinga na madhara yatokanayo na bidhaa zinazoteketezwa.

Zaidi ya tani 20 za dawa tofauti zimeangamizwa zikiwamo ambazo muda wa matumizi umepita zilizopatikana kupitia ukaguzi mbalimbali wa dawa bandia wiki iliopita.

# Kampuni yatakiwa kuwalipa wafanyakazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameuagiza uongozi wa kampuni ya Sino yenye makao makuu yake mchini China kuwalipa wafanyakazi wake wote stahiki zao ndani ya kipindi cha wiki moja.

Ametaka malipo hayo yaende sambamba na uwasilishaji wa vielelezo vyote vya mikataba kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja katika kipindi hicho. Heme amesema uongozi wa kampuni hiyo inaendesha kituo cha mradi wa kilimo cha umwagiliaji na ujezi wa barabara Kibokwa, Kaskazini Unguja, umekuwa ukiwasumbua na kuwanyanyasa wafanyakazi wazalendo. Aliyasema hayo jana alipofanya ziara yake katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na kukagua maendeleo na changamoto zinazowakabili wananchi. Hemed alisema serikali ya Zanzibar haitasita kumwondosha nchini ndani ya Saa 24 mkandarasi mkorofi anayewanyanyasa wananchi.

Aidha, alisema serikali haitomvumilia mkandarasi yeyote wa kigeni aliyepewa jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi na akashindwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa nchini. Makamu wa pili huyo aliwahakikishia wafanyakazi wazalendo wa kampuni hiyo kwamba hawataonewa tena kuanzia sasa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itasimamia suala hilo bila kumwonea mtu au taasisi yoyote.

Hata hivyo, aliwataka wafanyakazi hao baadhi yao kuacha tabia ya udokozi ikiwamo kunyonya mafuta ya vyombo vya moto, vinginevyo serikali kupitia vyombo vya dola haitasita kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo kufukuzwa kazi.

Naye Kamishna wa Kazi Zanzibar, Fatma Iddi Ali, alisema Sino imekuwa na matatizo mengi yanayosababisha kutokea kutoelewana kati yake na wafanyakazi ikiwamo usiri wa mikataba.

Fatma alisema sheria ya kazi iko wazi katika kuona mwajiri na mfanyakazi wake wanafikia makubaliano katika malipo yaani mishahara jambo ambalo kampuni ya Sino imeshindwa kukamilisha suala hilo la kisheria.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MÀHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI NO 76/2021
MADAI MICHAEL SABAS
DHIDI YA
MDAIWA PROSPER MICHAEL**

**KWA PROSPER MICHAEL**

**Ombi la Mdai MICHAEL SABAS
Madai ya pesa sh.1,725,000/=**
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauril tajwa hapo juu bila kukosa.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo **Tarehe 25 Mwezi 3 Mwaka 2021 saa 2:00** Asubuhi.
Angalia Kama hukuhudhuria/hamtohudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha Kama Umepokea/ Mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Màhakama hii leo **tarehe 16 Mwezi 03 Mwaka 2021**

**HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ELMON ALEXANDER MAHAWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA SPACIO** yenye namba za usajili **T 890 DGY** Chassis No. **NZE1213161675,** Engine **No.INZA620702.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi
**DSM/PHQ/RB/139263/2021**

**MBELE YA MAHAKAMA YA MWANZO:
MIKESE**

**MADAI NAMBA 3/2021**

**MDAI: MAGRETH A WANDU**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: KELLY MESHACK LUVAO**

**KWA: KELLY MESHACK LUVAO
MBEZI BEACH KINONDONI**

**Ombi la Mdai: MAGRETH A WANDU
Anadai: TALAKA MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri linalokukabili ambalo limetajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi 3 mwaka 2021.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MIKESE
IMETIWA SAHIHI LEO TAREHE 18/03/2021

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO.52/2021
Ombi la RESTITUTA STEPHANO NANDI kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu JUSTINE STEPHANO NANDI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 24/03/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo . Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 24/02/2021

Tarehe 24/2/2021
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

## VACANCY
**Secretary and Psychologist.**

Pour your heart Psychotherapy and counseling center. We are located at Palm Village Mall Mikocheni. We have a vacancy for the position of a Secretary and Psychologist. The secretary should have a diploma with good computer skills and The psychologist should hold at least a Bachelor degree and A year experience in the field.

**Send your CV over to info@pouryourheartnow.com or call 0764 885 881 / 0657 116 745.**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Wanamgambo wadaiwa kuua watoto

**Cabo Delgado,** MSUMBIJI

SHIRIKA la kimataifa limesema watoto wadogo hadi miaka 11 wanauawa kwa kuchinjwa na wanamgambo wa Kiislamu katika mkoa wa Cabo Delgado, Kaskazini mwa Msumbiji.

Mwanamke mmoja aliliambia Shirika la Save the Children, kwamba alishuhudia mtoto wake aliyekuwa na umri wa miaka 12 akiuawa karibu na mahali alipojificha na watoto wake wengine.

**Baada ya mwanangu kuuawa, tulibaini hii ni hatari kuendelea kuishi katika kijiji chetu.**

"Baada ya mwanangu kuuawa, tulibaini hii ni hatari kuendelea kuishi katika kijiji chetu," alisema.

"Tulikimbilia nyumbani kwa baba yangu katika kijiji kingine, lakini baada ya siku chache mashambulio yakaanza tena hapo."

Zaidi ya watu 2,500 wameuawa na wengine 700,000 wametoroka makwao katika mkoa wa Cabo Delgado ulio na utajiri mkubwa wa gesi na mafuta tangu mashambulio ya wanamgambo yalipoanza mwaka 2017.

Baadhi ya watu wamefariki wakijaribu kutoroka eneo hilo baada ya boti waliyokuwa wakisafiri kuzama.

Novemba, mwaka jana, chombo cha habari cha kitaifa kiliripoti kwamba zaidi ya watu 50 waliuawa kwa kuchinjwa katika uwanja wa mpira wa miguu mkoani humo.

Aprili mwaka jana, makumi ya watu walichinjwa na wengine kuuawa kwa kupigwa risasi katika kijiji kimoja.

Makundi ya kutetea haki yalidai vikosi vya serikali vimekuwa vikitekeleza ukiukwaji wa binadamu, ikiwa ni pamoja na kukamatwa kiholela, ukatili na mauaji wakati wa operesheni dhidi ya wanamgambo wa kijihadi.

Serikali ya Msumbiji imeomba jamii ya kimataifa kuisaidia kukabiliana na mashambulio ya wanamgambo. **BBC**




Waandamanaji wanaopinga mapinduzi ya kijeshi wakionyesha mabango walipokusanyika mjini Yangon, jana. Inakadiriwa maandamano hayo tangu yaanze nchini Myanmar yamesababisha vifo vya watu 138. **PICHA: AP**

## 4 wanyongwa Iran kwa ubakaji

**Mashhad,** IRAN

WANAUME wanne wamenyongwa nchini Iran kwa kumbaka mwanamke.

Taarifa hiyo iliripotiwa na mtandao wa habari wa YJC hapo juzi. Kwa mujibu wa wachunguzi, wanaume hao waliwateka nyara mtu na mkewe katika mji wa Sefid Sang, kaunti ya Fariman Kaskazini Mashariki mwa Iran mwaka uliopita.

Walimfunga mwanamume huyo na kumbaka mke wake mara kadhaa mbele yake.

Ripoti ya YJC, ilisema wanaume hao wanne walinyongwa jana katika gereza kuu la mji wa Kaskazini Mashariki wa Mashhad, baada ya mahakama ya juu kuruhusu hukumu ya kifo itekelezwe.

Hukumu ya kifo nchini Iran, hupitishwa kwa makosa ya mauaji, ubakaji, wizi wa kutumia silaha na ulanguzi wa dawa za kulevya, miongoni mwa makosa mengine.

Utekelezaji wa hukumu ya kifo huharakishwa kwa kesi za ubakaji na udhalilishaji wa watoto. **DW**

## UN: Waandamanaji 138 wauawa Myanmar

**New York,** MAREKANI

WAANDAMANAJI wasiopungua 138, wameuawa nchini Myanmar kufuatia maandamano ya nchi nzima tangu mapinduzi ya kijeshi kufanyika Februari Mosi, mwaka huu.

Hayo ni kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN).

Msemaji wa UN, Stephanie Dujarric aliwaambia waandishi wa habari mjini New York, juzi kwamba miongoni mwa waliouawa ni wanawake na watoto, akitaja takwimu kutoka Shirika la Umoja huo la Haki za Binadamu.

Alisema hali katika eneo la Kusini Mashariki mwa taifa hilo, imekuwa mbaya zaidi tangu mwisho wa wiki iliyopita wakati waandamanaji 18 walikiuawa Jumamosi na 38 Jumapili.

Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres alishutumu vikali machafuko yanayoendelea dhidi ya waandamanaji wa amani na kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuwasaidia raia wa Myanmar katika juhudi zao kutaka demokrasia kurejeshwa.

Guterres alisema juzi kwamba anasikitishwa na kuongezeka kwa ghasia nchini Myanmar na zinazofanywa na jeshi la nchi hiyo, kwa mujibu wa msemaji wake.

Serikali ya kijeshi ya Myanmar iliongeza muda wa sheria za kijeshi katika maeneo zaidi ya mji mkuu Yangon, Jumatatu, huku kukiwa na ripoti kwamba waandamanaji zaidi waliuawa na vikosi vya usalama.

Kundi la Utetezi la Wafungwa wa Kisiasa (AAPP), ambalo limekuwa likifuatilia ghasia za nchini humo, lilisema kwamba takriban watu 20 waliuawa Jumatatu katika mashambulizi ya risasi.

Televisheni ya serikali ya MRTV, ilitangaza kwamba wilaya za North Dragon, South Dragon, Dagon Seikkan, na North Okkalapa ziko chini ya sheria za kijeshi kutokana na maandamano ya mwishoni mwa juma ambayo yalikuwa mabaya. **VOA/DW**

## Ujerumani, Ufaransa, Italia zasitisha chanjo AstraZeneca

UJERUMANI, Ufaransa na Italia zimetangaza kusimamisha kutolewa chanjo ya AstraZeneca, baada ya ripoti kuonyesha uwezekano wa kuwa na madhara.

Licha ya kuwapo kwa madai ya aina hiyo ya chanjo kuwa na madhara Shirika la Afya Duniani (WHO), linadai kwamba chanjo hiyo ni salama. Nchi hizo, zinajiunga na nchi kadhaa wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) ambazo zimezuia kutolewa kwa chanjo ya AstraZeneca.

Nchi hizo zimeifuata uamuzi wa Norway, ambayo ilitangaza mwishoni mwa wiki kwamba mtu mmoja alifariki dunia baada ya kupata madhara katika ubongo na wengine watatu kulazwa baada ya damu kuganda mara tu ya kupewa chanjo ya AstraZeneca. **VOA**

# KOCHA WA LEIPZIG AIKATAA BARCELONA



**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann, amekanusha madai ya kuhusishwa na kwenda kuchukua nafasi hiyo katika timu ya Barcelona.

Nagelsmann ameripotiwa kwamba, anatakiwa kule Camp Nou na Rais mpya wa Barcelona, Joan Laporta, ambaye anaaminika kwamba anataka kumtema Ronald Koeman.

Leipzig pia amekuwa akihusishwa na kuchukua mikoba kwa mabingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich huku kukiwa na uvumi juu ya majaliwa ya Hansi Flick.

Lakini Nagelsmann amekanusha madai hayo na kusema kwamba, uvumi ni sehemu ya kawaida.

"Nina mawasiliano mazuri na Alfred (Schreuder - kocha msaidizi wa Barcelona), lakini si kwa mambo ya kazi," alisema kocha huyo mwenye umri wa miaka 33, akiwaambia waandishi wa habari.

"Na tunawasiliana kwa sababu alikuwa msaidizi wangu wakati nikiwa kocha kule Hoffenheim, na nina uhusiano naye mzuri sana.

# Klopp afunguka ushindi kwa Wolves

**LONDON,** England

JURGEN Klopp ameshereheka 'pointi tatu chafu' baada ya Liverpool kupambana vikali na kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Wolves katika Uwanja wa Molineux.

'Wekundu' hao walipata ushindi wao wa pili mfululizo kwenye Ligi Kuu tangu Januari, wakiwa pia wametoka kupata ushindi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita na wakapata bao hilo pekee kwenye mchezo huo likifungwa na Diogo Jota.

Na ingawa timu haikuwa kwenye kiwango chake bora, Klopp aliridhika na namna wachezaji wake walivyocheza.

"Lilikuwa pambano kubwa. Pointi tatu chafu, na hivyo ndivyo tunavyotakiwa kurudi kwenye njia yetu," alisema Klopp akiiambia Sky Sports.

"Tulikuwa na wakati mzuri, tulikuwa na wakati ambao tulijilinda vizuri, kwa hakika tulicheza kwa kupambana sana.

"Sikupenda mwanzo wetu, hatukufanya vizuri sana na baadaye tukabadilika na kucheza vizuri."





# Halaand kipaumbele kwa Man U

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imemfanya nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland kama kipaumbele chao cha umsajili kipindi cha majira ya joto, kwa mujibu wa Manchester Evening News.

United walijaribu kumsajili Haaland mwenye umri wa miaka 20, kabla ya kujiunga na Dortmund akitokea kwa mabingwa wa Austria, Salzburg mwaka jana.

Na sasa 'Mashetani Wekundu' hao wanataka kumchukulia Haaland ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji msimu ujao.

Man United hadi sasa bado hawajaziba pengo la Romelu Lukaku, huku pia mkongwe Edinson Cavani akihusishwa na Boca Juniors kwani mkataba wake wa mwaka mmoja unafikia mwisho kipindi cha majira ya joto.

Mkurugenzi wa soka wa Man United, John Murtough, ameripotiwa kwamba amemkubalia kocha Ole Gunnar Solskjaer kumwania Haaland kwa ajili ya usajili wa kipindi cha majira ya joto.

Haaland pia amekuwa akihusishwa na Real Madrid, Barcelona, Chelsea, Liverpool, Manchester City, Paris Saint-Germain na Juventus.

## HABARI MICHEZO

# Tuchel aweka kwanza usajili kando Chelsea

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesisitiza kuwa hajaona mshambuliaji mpya atakayekuja msimu juo na anaamini si muda sahihi wa kufikiria masuala ya usajili kwa sasa.

Chelsea imecheza mechi 12 chini ya Tuchel bila kupoteza na Giroud ndiye mshambuliaji aliyefunga mabao mengi zaidi chini yake akiwa na mabao mawili.

Nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, anapigiwa upatu kuwa ndiye chaguo namba moja kwenda kuongeza makali katika safu ya ushambuliaji ya Chelsea.

Lakini Tuchel hafikiri kuhusu usajili kwa sasa, kwani muda muafaka bado haujafika kwake.

"Sio wakati wa kutafakari kuhusu majira ya joto na suluhisho zingine, zaidi ya yale tuliyo nayo," alisema Tuchel akinukuliwa na BBC Sport.

"Tuna wachezaji ambao tunafurahia nao na tunatafuta suluhisho zaidi, tutajaribu kuwasaidia.





# RONALDO: NATAKA REKODI ZAIDI DIMBANI

**TURIN,** Italia

NYOTA wa Juventus, Cristiano Ronaldo, amesema mara zote anataka "zaidi na zaidi" wakati akikodolea macho rekodi nyingine baada ya kuizima ile ya Pele.

Ronaldo alifunga mabao matatu 'hat-trick' Jumapili na kuiwezesha Juve kupata ushindi wa 3-1 dhidi ya Cagliari kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, na kufikisha mabao 770, akimpita Pele matatu.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or sasa amekuwa mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi kwenye historia ya soka kwa kumzidi gwiji huyo wa Brazil, Pele.

"Bado kuna mengi zaidi ya kuyafikia na nafikiri tunaweza kufanya pamoja," aliandika Ronaldo kupitia ukurasa wake wa Instagram.

"Mabao ni sehemu muhimu kwa nilivyo sasa. Siwezi kuacha kuendelea kutafuta mafanikio zaidi na zaidi na kupata rekodi nyingi zaidi.

"Mara zote nataka zaidi na zaidi na nafikiri ndio maana watu wanasema nina nguvu nyingi sana na kamwe siwezi kuacha.

"Pengine ni kweli, lakini mafanikio haya yananifanya mimi niendelee kuwa kwenye kiwango changu bora."

# Greenwood kuichezea England kikosi cha U-20

**LONDON,** England

NYOTA wa Manchester United, Mason Greenwood, amejumuishwa kwenye orodha ya wachezaji wa timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 20, watakaocheza mashindano ya Euro 2021 kwa umri huo.

Greenwood ambaye ameshaichezea timu ya wakubwa ya England mara moja, amejumuishwa kwenye kikosi cha kocha, Aidy Boothroyd na atacheza hatua ya makundi mwishoni mwa mwezi huu.

Haya ni matokeo ya kiwango bora ndani ya kikosi cha United kwa siku za karibuni ambapo Mason Greenwood amekuwa akiendelea kujiimarisha zaidi katika nafasi ya ushambuliaji.

England wapo Kundi D ambapo watachuana na Uswisi Machi 25, Ureno (Machi 28) na Croatia (Machi 31).

Mashindano ya Euro 2021 chini ya umri wa miaka 20, yatachezwa katika nchi mbili za Hungary na Slovenia.

Hatua ya mtoano itaanza kutimua vumbi Mei na Juni wakati fainali itachezwa Juni 6, mwaka huu katika Mji Mkuu wa Slovenia, Ljubjana.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AIFIKIA REKODI YA XAVI BARCELONA

**Ni heshina kubwa kufikia idadi hii ya mechi hapa Barca, shukrani kwa wachezaji wenzangu...**

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi ameifikia rekodi ya Xavi ya kuichezea mechi nyingi zaidi Barcelona wakati akiisaidia kupata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Huesca kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumatatu.

Messi sasa amefikisha mechi 767 alizoichezea Barcelona kwenye mashindano yote na kuwa sawa na Xavi - ingawa yeye anaweza kutengeneza rekodi mpya kwenye mchezo wa Jumapili dhidi ya Real Sociedad.

Messi mshindi mara sita wa Ballon d'Or alikuwa nyota wa mchezo huo pale Camp Nou, akifunga mabao mawili na kutengeneza bao la Oscar Mingueza.

**Mabao yake mawili yamemfanya kutingisha nyavu mara 21 msimu huu kwenye LaLiga, huku 14 kati yake akifunga kuanzia Januari Mosi hadi sasa.**

Pia Messi aliweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kwenye Historia ya LaLiga kufunga mabao 20 katika misimu 13 mfululizo.

Baada ya mchezo huo, Messi aliandika kupitia ukurasa wake wa Instagram: "Ni heshina kubwa kufikia idadi hii ya mechi hapa Barcelona.

"Shukrani kwa wachezaji wenzangu kwa sapoti yao kwa kipindi chote cha miaka niliyocheza hapa, pamoja na sapoti ya familia yangu na mafariki."

## ZISIKUPITE

### DYBALA AWANIWA EPL

TOTTENHAM na Chelsea zimeripotiwa kuwania kumsajili straika wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 27, kutoka Juventus. ***(France Football, via Sport Witness)***

### MESSI ASITAJWE PSG

KIUNGO wa Paris St-Germain, Leandro Paredes amethibitisha kwamba, aliambiwa na mabosi wa klabu hiyo "kutozungumza kuhusu Lionel Messi" wakati huu nyota huyo wa Barcelona mwenye umri wa miaka 33, akihusishwa na uhamisho wa kutua kwenye timu hiyo. ***(Le Journal du Dimanche)***

### WERNER CHAMBO KWA HAALAND

CHELSEA inafikiria kumjumuisha mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, kama sehemu ya kukamilisha dili la usajili wa nyota wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20. ***(Football Insider)***

### AUBAMEYANG KUFUATWA

STRAIKA wa Hatayspor, Aaron Boupendza mwenye umri wa miaka 24, anataka kuhamia kwenye Ligi Kuu England na anawaniwa na klabu za Southampton, Tottenham, Leicester, West Ham, Newcastle United, Crystal Palace na Wolves. Boupendza ambaye ni mchezaji mwenzake na Pierre-Emerick Aubameyang kwenye timu ya Taifa ya Gabon, pia anahusishwa na Arsenal. ***(90 min)***

### MAN UNITED NA HALAAND

MANCHESTER itamfanya Erling Haaland kama kipaumbele chao cha usajili wa kipindi cha majira ya joto, na wameachana na mpango wa kumwania straika wa Tottenham, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27. ***(Manchester Evening News)***

### DEMBELE KUPEWA MKATABA

BARCELONA wapo tayari kutoa ofa ya mkataba mpya kwa straika wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 23, ambaye awali alihusishwa na mpango wa kwenda Manchester United. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### ARSENAL KUMBAKIZA ODEGAARD

ARSENAL wanaangalia uwezekano wa kumbakisha kiungo wa Real Madrid, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 22, pale kwenye dimba la Emirates msimu ujao, anapocheza kwa mkopo hapo kwa sasa. ***(Mail)***

### RUDIGER AONGEZEWA MKATABA

CHELSEA imemwongezea mkataba mpya, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, kabla ya kuanza kwa michuano ya Euro ili kuepuka kumruhusu kuingia kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake. ***(Mail)***

### ZIDANE NA RONALDO MADRID

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amesema kwamba, taarifa kuwa nyota wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, anataka kurudi katika klabu hiyo zinaweza kuwa kweli. ***(Sky Italia, via Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Washambuliaji New King tatizo - Dunia

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya New King, Ame Dunia, amesema kukosa umakini kwa washambuliaji wake kumekuwa chanzo cha timu hiyo kushindwa kupata mabao ya kuwapa ushindi.

Dunia ameyasema hayo juzi baada ya kumalizika kwa mchezo kati ya timu yake na Mchangani United uliomalizika kwa sare ya bao 1-1 katika mfululizo wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.

Alisema awali alizani kuwa tatizo ni uwezo wa timu kutozoea daraja wanalocheza kwa kuwa wamepanda msimu huu, lakini kumbe ni wachezaji kupoteza umakini pindi wanapolikaribia lango la wapinzani wao.

Kocha huyo alisema licha ya kujaribu kufanyia kazi udhaifu huo, lakini inaonekana bado washambuliaji hawajatuliza akili zao pindi wanapokuwa eneo zuri la kufunga.

"Washambuliaji ndio tatizo, mfano mchezo wetu huu tumekosa mabao mengi sana tena ya wazi, mengine ni kipa na mfungaji tu, lakini mipira inatoka nje," alisema.

## Netiboli Afrika kupigwa Julai

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya mchezo wa netiboli kwa Mataifa ya Afrika yanatarajiwa kufanyika mwanzoni mwa Julai hadi Agosti, mwaka huu nchini Namibia, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Netiboli Tanzania, Devota Marwa, alisema mashindano hayo yatafanyika endapo, maambukizo ya virusi vya corona yanayosababisha ugonjwa wa COVID-19, yatapungua kwa kuwa nchi nyingi bado mipaka yao imefungwa.

"Tunawasiliana mara kwa mara na viongozi wa timu za Namibia kuelekea kwenye mashindano hayo. Wanatuambia wanaendelea kujiandaa huku wengi wakiomba ugonjwa huu uishe ili majukumu mengine yaendelee," alisema Devota.

Alisema kuibuka kwa ugonjwa wa COVID-19 kumeharibu mipango mingi ambayo walikuwa wameipanga katika kipindi cha mwaka 2021, kutokana na baadhi ya shughuli kusimama.

# KIM, KASEJA WATOA SABABU KIPIGO STARS KWA HARAMBEE

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Harambee Stars ya Kenya, Kocha Mkuu wa timu ya Soka ya Tanzania, Taifa Stars, Kim Poulsen, amesema makosa binafsi kwenye safu ya ulinzi ndiyo yaliyosababisha kupoteza mechi hiyo.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyayo nchini Kenya, kocha huyo aliyeichukua timu hiyo hivi karibuni kutoka kwa Mrundi Etienne Ndayiragije, alisema ilikuwa nzuri na Harambee Stars waliwapa pambano zuri la kuangalia sehemu gani pa kurekebisha..

"Wametupa mechi nzuri. Mechi ilikuwa muhimu, tulitaka kuona wachezaji wetu wanacheza. Tatizo ni kwamba hatukuzuia vizuri, tumepoteza kwa makosa binafsi," alisema kocha huyo.

**Hata hivyo, alisema hiyo huwa inatokea hasa kuwa na wachezaji wapya ambao hawana uzoefu kwenye timu ya taifa, hivyo watakwenda kusawazisha baadhi ya makosa, kuangalia kwenye mechi nyingine dhidi ya Harambee Stars, kesho.**

Kwa upande wa kipa Juma Kaseja, alisema mechi ilikuwa nzuri na walicheza vizuri kuliko wapinzani wao, tatizo kubwa ni kwamba wamepoteza.

"Kilichotuhukumu ni matokeo tu, lakini hata umiliki wa mpira sisi tulikuwa juu, kwa hiyo tunarudi kwenye uwanja wa mazoezi kurekebisha makosa," alisema.

Aliwasifu wachezaji wa Stars kwa kucheza vema, licha ya kwamba wengi ni wapya, na kwamba kama wakiunganika na kundi lingine ambalo litajiunga baadaye, kikosi hicho kitakuwa moto.

"Timu inajengwa, wachezaji wengi ni vijana, lakini wameonyesha kuwa kuna jambo. Huko mbele itakuwa timu nzuri sana," alisema kipa huyo aliyefungwa bao moja kipindi cha kwanza.

Stars itarudiana na Harambee Stars kesho Alhamisi kwenye Uwanja wa Moi Kasarani nchini Kenya. Hizo ni mechi za kirafiki za kimataifa, Stars ikijiandaa na mechi za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika(Afcon) dhidi ya Equitorial Guinea Machi 25 ugenini, huku siku tatu baadaye ikicheza dhidi ya Libya Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**SOKA MEZANI...**




Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Zantel, Aneth Muga, akicheza mchezo wa soka kwenye meza na Issa Chapu, wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya 'Pasua Anga Ki Zantel 4G', uliofanyika katika viwanja vya Kisonge Unguja, Zanzibar. Kampeni hiyo imelenga kuwaelimisha wateja juu ya umuhimu wa mtandao wa 4G katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. **MPIGAPICHA WETU**

# *Baraza aanika mikakati Kagera Sugar*

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Biashara United, Mkenya Francis Baraza, leo anatarajia kutua mkoani Kagera kuanza kuitumikia rasmi timu hiyo, kwa mkataba wa miaka miwili na nusu, huku akianika mikakati kibao aliyokwenda nayo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema ameamua kuhama katika klabu yake ya awali, Biashara United na kwenda kuitumikia timu ya Kagera Sugar, kwa lengo la kubadilisha mazingira.

Baraza alisema timu hiyo haitapumzisha licha ya Bodi ya Ligi ya Tanzania kutoa mapumziko ya wiki tatu kwa ajili ya kupisha majukumu ya timu ya taifa, na kusema ataendelea na mazoezi ili kuzidi kuwaweka sawa kuelekea kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na Kombe la FA.

"Ninaripoti rasmi katika uongozi wa Kagera kwa ajili ya kuanza kazi ya kuitumikia timu yangu, lengo langu ni kuhakikisha naiweka mahali pazuri timu yangu na katika hilo nitawapa wachezaji mbinu zitakazowalinda na adui yeyote uwanjani," alisema Baraza.

Baraza alisema ataipambania timu hiyo ibaki Ligi Kuu licha ya msimu huu kuwa na ushindani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu kutokana na kuhofia isishuke daraja.

Alisema baada ya kukabidhiwa mikoba ya kuifundisha timu hiyo, atawapa wachezaji mapumziko ya siku tatu tu, kisha warudi kambini kuendelea na mazoezi, akidai Kagera Sugar ni miongoni mwa timu nzuri ambayo wachezaji wake wanajituma wanapokuwa uwanjani.

Aidha, alisema baada ya kuisoma timu hiyo kupitia baadhi ya michezo ya Ligi Kuu aliyoifuatilia, amebaini udhaifu mdogo ulioisababishia kutofanya vema na kuwa kwenye nafasi mbaya, lakini ameahidi ataufanyia kazi ili ligi itakapoanza, wachezaji wawe na mbinu mpya.

Baraza anaipokea Kagera Sugar ikiwa katika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kushuka dimbani mara 24 na kujikusanyia pointi 25.

# Michezo

Jumatano Machi 17, 2021

Nipashe




Messi aifikia rekodi ya Xavi Barca UKURASA 22

SOGEA UONE...




Winga wa Simba, Bernard Morrison, akipiga hesabu kumtoka beki wa timu ya Al-Merrikh kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo waliibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Simba sasa tishio Afrika

## Bado pointi moja tu kutinga robo fainali CAF, Morrison na Miquissone acha kabisa, refa apata corona...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABAO ya kiungo mshambuliaji Luis Miquissone, beki Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na straika Chris Mugalu, yameifanya timu ya Simba kukaribia kabisa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi kwa kuikandamiza Al-Merrikh ya Sudan mabao 3-0 jana jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ushindi huo unamfanya Kipa wa timu hiyo, Aishi Manula kuendelea kuonyesha uhodari wake baada ya kucheza mechi ya tatu ya hatua ya makundi bila kuruhusu bao wakati huu Simba ikiwa kileleni mwa msimamo wa Kundi A na pointi 10 ikifuatiwa na Al Ahly ya Misri yenye alama saba, ambayo nayo jana iliichapa AS Vita 3-0 nchini DR Congo, hivyo kuwafanya Wakongo hao kubaki na pointi nne huku Al-Merrikh ikiburuza mkia kwa pointi yake moja.

Mechi hiyo ilianza taratibu kwa kila timu kujaribu kusoma mbinu za mwenzake, lakini Al-Merrikh ikionekana kukaa nyuma zaidi na kuicha Simba ichezee mpira. Hata hivyo, wachezaji wa Simba walishindwa kabisa kutumia nafasi ambazo zilikuwa zinapatikana hadi ilipotimu dakika ya 17, ilipoandika bao la kwanza.

Alikuwa ni yule yule aliyeisulubu Al Ahly, Miquissone raia wa Msumbiji alipokwamisha mpira, baada ya kazi nzuri iliyofanywa na Mghana Bernard Morrison ambaye alikuwa kwenye kiwango bora kabisa jana.

Morrison kwa mara nyingine, alimchungulia 'Zimbwe Jr', akammiminia pasi ndefu iliyomkuta beki huyo Zimbwe Jr, akiwa kwenye winga ya kushoto, lakini aliupiga mpira kwa ufundi na kuujaza wavuni dakika ya 38, akimuacha kipa Monged Abdulzaid akilaumu mabeki wake.

Beki Joash Onyango alilazimika kutolewa dakika za mwishoni mwa kipindi cha kwanza kutokana na maumivu yaliyotokana na kupigwa na mpira kichwani, nafasi yake ikachukuliwa na Erasto Nyoni.

Dakika ya 49, Simba iliandika bao la tatu lililofungwa na Mkongomani Mugalu, aliyepokea kwa kifua krosi kali kutoka kwa Miquissone, kabla ya kuachia shuti kali lililokwenda moja kwa moja wavuni.

Simba iliwatoa Mzamiru Yassin, Mugalu, Miquissone, na Morrison, nafasi zao zikichukuliwa na Rally Bwalya, Francis Kahata, Meddie Kagere na Jonas Mkude, ambapo walichokifanya ni kuhakikisha timu inamiliki mpira zaidi na kuwanyima nafasi wapinzani kuwashambulia.

Clatous Chama alikosa bao dakika ya 82, na dakika chache baadaye Al-Merrikh walionekana kuchachamaa na kufanya mashambulizi makali mawili ambayo nusura yawapatie bao kupitia kwa straika wao hatari na mwenye nguvu, Saif Terry lakini uimara wa kipa Manula, uliinusuru Simba kuruhusu bao.

Katika hatua nyingine, mechi hiyo haikuwa na mwamuzi wa mezani kwa kile kilichodaiwa kuwa alikutwa na maambukizi ya corona, hivyo kazi yake ilikuwa ikifanywa na mshika kibendera namba moja kila timu ilipokuwa ikitaka kufanya mabadiliko na kuonyesha muda uliosalia na wa dakika za majeruhi. Hiyo inakuwa mechi ya kwanza katika rekodi ya Simba kushinda nyumbani bila mashabiki baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutoa agizo hilo huku ikiruhusu mashabiki 200 tu ambao walionekana kufanya kazi ya ziada kushangilia wakisaidiana na Ofisa Habari wa timu hiyo, Haji Manara.

Kwa matokeo hayo inahitaji pointi moja tu katika mechi zake mbili dhidi ya AS Vita (Aprili 2-3) katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na ili kufuzu hatua ya robo fainali kabla ya kuhitimisha na Al Ahly nchini Misri kati ya Aprili 9-10, mwaka huu.

# Mfaransa Yanga sasa ni muda tu

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya Klabu ya Yanga kusema kuwa imekuwa ikipokea barua za kuomba kazi na wasifu (CV) kutoka kwa makocha mbalimbali duniani, akiwamo Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Sudan, Mfaransa Hubert Velud, si siri tena kwani mzaliwa huyo wa Villefranche-sur-Saone, Ufaransa ndiye amelamba dume kuinoa.

Hata hivyo, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, hakutaka kuweka wazi mapema suala hilo baada ya kumweleza mwandishi wetu kuwa, kazi ya kusaka kocha wa timu hiyo anayetarajia kuanza kazi kuanzia msimu ujao inafanyika kwa umakini mkubwa, huku wakiendelea kupokea CV kutoka kwa makocha mbalimbali ndani na nje ya Afrika.

Mfikirwa alikiri kupokea barua na wasifu kutoka kwa Kocha Mkuu huyo wa timu ya Taifa ya Sudan, Velud, lakini hakuwa tayari kusema ndiye aliyelamba dume kuinoa kuanzia msimu ujao.

"Ni kweli kocha huyo ni mmoja wa makocha aliyetuma CV yake na kuomba kazi, na siyo huyo ni wengi sana na siyo kama kwa sababu ametuma yeye basi ndiyo amepata kazi, hapana. Sisi tunapokea barua hizi kutoka kwa Kamati ya Ufundi, na baada ya hapo nasi pia tuna vigezo vyetu mbalimbali ambavyo tunahitaji kwa kocha wa timu yetu kuwa navyo. Yoyote atakayetimiza basi ndiye atakuwa amepata nafasi hiyo," alisema katibu huyo.

Lakini chanzo chetu ndani ya kamati hiyo ya utendaji kilieleza: "Jina ambalo limekubalika ni la Velud, muda tu ndio utaongea, tusubiri."

Kwa sasa Yanga imemtangaza Juma Mwambusi kuwa ndiye Kaimu Kocha Mkuu mpaka mwisho wa msimu, akichukua nafasi ya Mrundi Cedric Kaze aliyetimuliwa hivi karibuni kutokana na mwenendo usioridhisha wa matokeo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >